




UKURASA 24

**FATMA KARUME** ajitosa kesi ya Yanga na Fei Toto


Ukurasa 12
NI KAMA SIMULIZI YA KUSADIKIKA ... Mjasiriamali mwenye ulemavu kapambana hadi kusimama, leo ana ofisi na ameajiri

Ukurasa 13
Serikali imtazame Osam Milanzi kwa jicho la tatu

BUFE
IJUMAA MACHI 3, 2023
Nipashe

Ukurasa 14
Moto wawaka Baraza la Madiwani Magu, kashfa kupotea mabati kwenye kituo afya

DEREVA BAJAJI MZEE JULIUS MILAMBO...
Mtumishi umma aliyesota mahabusu miaka kibao, kutoka anafikia kustaafu

Na Neema Hussein, Mpanda

MAISHA mara zote yanatajwa ni 'safari ndefu; unajua unakotoka si uendako. Mzee Julius Milambo (61) katika safari yake, alikuwa mtumishi wa umma, akakwama gerezani, anapokomboka mahabusu, akakuta ajira imetamati, sasa ni mstaafu anayeendesha bajaji.

Mzee huyo ni mkazi wa Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi, ambaye katika mazungumzo yake na Nipashe, anasimulia alikuwa mtumishi wa Halmashauri ya mkoa wa Katavi.

Anakumbuka alianza katika utumishi wakati wa mfumo wa chama kimoja kushika ...

hatia, nikawa nimeachiwa.

"Kukaa kule mahabusu, kumenisaidia kuwa inatakiwa niishi vipi na jamii na usikae tu ukabweteka, lazima utafute kazi ya kufanya," anasimulia.

Mzee Milambo anasema, baada ya kutoka mahabusu familia yake aliikuta iko chini sana kimaisha, wakati huo mke wake alikuwa akichoma vitumbua na kuuza mchele sokoni.

Anasema watoto aliowaacha wakiwa wanasoma shule ya awali, aliwakuta darasa la sita na mwingine aliyekuwa shule ya msingi alikuwa sekondari.

UKURASA 11


# Nipashe

Ijumaa Machi 3, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581238

MWANGA WA JAMII


www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Rais Samia: Kuna tatizo la uongozi

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na viongozi wa serikali kabla ya kufungua mkutano wa faragha jijini Arusha jana. **PICHA: IKULU**




Kamishna wa Polisi Zanzibar, Hamad Khamisi Hamad, akionyesha kitabu cha kanuni za mwongozo wa utendaji kazi wa jeshi hilo, wakati akizungumza na Nipashe jana kuhusu tuhuma za askari kujihusisha na vitendo vya ushoga. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# CCM yafungua mafaili ya wanaojipitisha majimboni

UKURASA 5

# KAMISHNA POLISI: Ikithibitika askari tunayemchunguza ni shoga, kazi hana kisha kizimbani

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA YATINGA ROBO FAINALI FA UK. 24

**KATUNI** UK. 6

# Anayetuhumiwa kuua mke, mtoto afikishwa kortini

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MTUHUMIWA August Matemu, amefikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi, akikabiliwa na mashtaka mawili ya mauaji ya mke wake na mtoto.

Akisoma mashtaka hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Jenipher Edward, Wakili wa Serikali, Kassimu Nasir, alidai kuwa Februari 22, mwaka huu, Kijiji cha Mamba Mero, Kirua Vunjo, mshtakiwa anadaiwa kumuua kwa kukusudia mke wake, Fausta Tesha akiwa amelala kwenye nyumba walipokuwa wakiishi.

Wakili Nasri alidai katika kosa la pili, siku hiyo hiyo, August anadaiwa kutekeleza tukio lingine la mauaji kwa makusudi kwa mtoto, Rodrigo Mgaya.

Kwa mujibu wa Wakili Nasri, upelelezi wa shauri hilo bado haujakamilika.

Hakimu Mkazi, Jeniffer alisema kesi hiyo haina dhamana huku akimtaka mshtakiwa kutojibu chochote mbele ya mahakama hiyo kwa kuwa, haina uwezo wa kusikiliza kesi hiyo.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Machi 22, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.



Mtuhumiwa wa mauaji ya mke wake na mtoto, August Matemu (katikati), akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi huku akishikiliwa na baba yake mzazi, John Bosco (kulia) na baba mkubwa, Finuel Patro (kushoto), baada ya kufikishwa kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: MARY MOSHA**

# Rais Samia asema kuna tatizo la uongozi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema pamoja na Tanzania kupiga hatua kwenye siasa safi, kuwa na ardhi ya kutosha na watu lakini kuna shida kwenye uongozi bora.

Aliyasema hayo jana jijini hapo wakati wa kikao kazi kilichowakutanisha viongozi wa serikali wakiwamo mawaziri, manaibu wazari, makatibu wakuu na manaibu katibu wakuu.

"Ndugu washiriki karibuni sana kwenye kikao kazi ambacho lengo kuu ni kukumbushana na kueleweshana juu ya kutimiza ipasavyo wajibu tulionao na dhamana tuliyoibeba ya kuwatumikia wananchi.

"Baba wa Taifa (Julius Nyerere) aliwahi kutueleza kuwa ili taifa letu liendelee tunahitaji mambo manne nayo ni watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora.

"Mtakubaliana nami watu tunao wa kutosha idadi yetu ni milioni 67, ardhi tunayo tena kubwa ingawa tuna migogoro kadhaa, siasa safi na yenyewe ipo kwasababu tunapotoka nje ya nchi sifa tunazopata ni kutokana na siasa safi tuliyonayo.

"Suala hapa lenye shida labda ni uongozi bora sasa hili tutakwenda kuliangalia hapa na kulijadili, tujifunze mambo yanayomfanya kiongozi awe bora ili tuisaidie nchi yetu.

**MIGOGORO**

Alisema kutokufanyika vikao kazi kwa muda mrefu kumesababisha athari serikalini zinazoonekana wazi katika utendaji kazi wa viongozi wa wizara mbalimbali na kuwapo kwa ombwe la uelewa wa utaratibu wa utendaji kazi serikalini.

Alisema hali hiyo inasababisha migongano isiyokuwa ya lazima kwa viongozi hao na kuathiri utendaji kazi na uwezo wa kuwahudumia wananchi.

Vilevile, alisema sababu hiyo imechangia viongozi kubadilishwa mara kwa mara, ili kuepusha serikali na fedheha ya kuwa na viongozi wanaoifanya wizara kuwa sehemu ya malumbano na migawanyiko isiyokuwa na tija.

"Ninafahamu madhara ya kubadilisha viongozi mara kwa mara na sipendi kufanya hivyo kwa sababu kunafanya watu wafanye kazi kwa hofu na viongozi wasiwe na mipango ya muda mrefu kwa kuhofia teuzi zao kutenguliwa," alisema Rais Samia.

Alifafanua kuwa kiongozi anapotolewa kazini ni fedheha kwa familia yake, watoto na vijiana ambao walikuwa wakimwona kama mtu wa mfano kwao.

"Mimi sio lengo langu kubadilisha viongozi mara kwa mara kwa kuwa huchukua muda mrefu kuwajenga hata na wakati mwingine ninalazimika kufanya hivyo ili kuepusha madhara kutokea zaidi serikalini na kwa wananchi."

Matumaini yake ni kuwa mkutano huo, utawaongezea ujuzi katika uongozi na utasaidia kuboresha utendaji kazi, kuondoa migongano na kuleta ufanisi na tija katika kutoa huduma kwa wananchi.

"Viongozi wazoefu ndio wanafanya viongozi wapya kuwaiga wakijua kwamba kuwa na migogoro, kutokufuata sheria utaratibu ni jambo la kawaida serikalini.

Kadhalika, Rais Samia alisisitiza suala mgawanyo wa majukumu, mipaka ya madaraka kwa viongozi hao, dhana ya uongozi na sifa ya kuwa kiongozi bora.

"Nimekuwa nikisisitiza kila wakati nyinyi kwa pamoja ni timu moja ya uongozi na utawala katika wizara kama viongozi mnategemewa kuonyesha njia kubuni nini kifanyike katika kutekeleza majukumu ya wizara mlizokabidhiwa kuziongoza kwa kufuata sheria, kanuni, miongozo na utaratibu wa serikali tuliojiwekea."

Aliwakumbusha viongozi jukumu la utawala wanategemewa kuwa makini na mahiri katika kusimamia kutumia rasilimali watu, vifaa na fedha za umma, pamoja na kuwa na mipango na mikakati thabiti ya kutekeleza na kusimamia majukumu hayo.

"Ili muweze kutimiza kwa ukamilifu wajibu wenu hamna budi kutambua vyema mipaka yenu ya uongozi na mamlaka na njia nzuri ya kuyajua haya ni kwa kusoma miongozo ambayo wanapatiwa baada ya kuteuliwa na kula kiapo," alisema.

**MAOFISA HABARI BINAFSI**

Aliwataka viongozi wa serikali kusemea mambo mazuri na mafanikio yaliyofikiwa na serikali badala ya kutoa nafasi kwa baadhi ya watu wasiokuwa na nia njema kufanya upotoshaji.

"Viongozi tumekuwa wazito kusemea mafanikio mengi tunayoyapata hivyo kuacha watu wengine kuendelea kufanya upotoshaji na kuna msemo unaosema uongo ukisemwa mara nyingi unageuka kuwa ukweli."

Amesema serikali imefanya mambo makubwa yaliyosaidia kutatua shida na kero za wananchi na kwamba ni wajibu kwa viongozi hao kutoa taarifa jinsi serikali ilivyotatua shida hizo.

"Nimewahi kuona kiongozi mmoja wa kisiasa akiilaumu serikali kwamba inatumia fedha nyingi kutafuta vyanzo vipya vya maji kupeleka kwa wananchi, lakini kuna visima kadhaa vilichimbwa nyuma na vimeachwa na tunatumia fedha nyingi kupeleka maji kwa wananchi.

"Ni kiongozi huyu huyu ambaye kuna kipindi yeye mwenyewe alisema kwa mfano hapa Arusha kulichimbwa visima vingi, lakini maji yote yalikuwa na chumvi hayakufaa kutumika kwa matumizi ya binadamu.

"Sasa kiongozi huyu huyu anasema serikali imeviacha visima na tumekwenda kutumia pesa nyingi kufutafuta vyanzo vingine na kupeleka maji kwa wananchi."

Alisema wizara inayohusika na jambo hilo ilitakiwa kujitokeza haraka kutoa majibu yenye ukweli, takwimu halisi na kumweleza mhusika kwa nini visima hivyo vimeachwa au havikuachwa.

"Nakumbuka wakati wa shida ya maji Mkoa wa Dar es Salaam ni visima hivi hivi ambavyo viliwekwa akiba viliwafaa wananchi, sasa mambo kama hayo kuweni wepesi wa kutoa majibu mnapomsikia mtu anapotosha na huu ni mfano mmoja, lakini iko mingi ya aina hii hivyo muwe wepesi wa wizara zenu kutoa taarifa.

"Najua kila wizara ina vitengo vya habari, je vinatumikaje au viko tu vimekaa havifanyi kazi, lakini bado baadhi ya mawaziri mmeajiri maofisa wenu wa habari binafsi wa kutoa taarifa zenu na sio za serikali, sasa mambo kama haya twendeni tukarekebishe na nimatumaini yangu kuwa mada kuhusu suala hili itatukumbusha wajibu wetu kama viongozi na wasemaji wakuu wa wizara zetu," alisema.

Alisema utoaji wa taarifa unapaswa kuzingatia kanuni na utaratibu, ili kuepuka kutoa taarifa zinazokinzana ndani ya taasisi moja na serikali moja.

HABARI KITAIFA

# Kamishna: Ikithibitika askari tunayemchunguza shoga kizimbani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMISHNA wa Polisi Zanzibar, Hamad Khamisi Hamad, amesema wanamchunguza askari wao anayetuhumiwa kwa ushoga na ikithibitika, atafukuzwa kazi na kushtakiwa mahakamani.

Akizungumza na Nipashe jana ofisini kwake mjini hapo, Kamishna Hamad alitaja sababu tatu za kutokukubaliana na tendo hilo ndani ya polisi; kinyume cha sheria, maadili na linalomwondolea ukakamavu askari.

Kutokana na mkasa huo, Kamishna Hamad aliyeonekana kukereka nalo, aliiambia Nipashe kwamba ofisi yake ina mpango maalum wa kuwasaka askari wake wote wenye hulka na kujihusisha na matendo ya aina hiyo.

"Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wa kadhia hiyo ikiwamo kufanyiwa kipimo askari huyo ili kujiridhisha kama kweli anafanya kitendo hicho... ingawa tumeona video katika mitandao ya kijamii lakini hatuwezi kusema moja kwa moja kama ni kweli au sio kweli," alifafanua.

Alisisitiza kwamba, kanuni na mwenendo wa kisheria za jeshi hilo haziruhusu mapenzi ya jinsia moja, na madai hayo yakithibitika, atafikishwa kwenye mahakama ya kijeshi na hatua nyinginezo.

Kamishna Hamad alisema askari anapokuwa shoga, hukosa uaminifu na ukakamavu katika jukumu lake la msingi la kulinda raia na mali zao.

"Hatufai na atashindwa kufanya kazi za polisi, na hata heshima kwa jamii haitakuwapo. Kama unamtuma askari polisi wa aina hii akamkamate mhalifu, akifika huko anaweza hata akaguswa (....). Sasa heshima iko wapi kwa Jeshi la Polisi?" alilalamika katika kauli ya kukereka.

Aliendelea: "Huu si utamaduni wa Jeshi la Polisi na wala hakutumwa hivyo. Matendo ya mtu binafsi lazima yatafautishwe na taasisi.

"Hata hizo picha zinazosambaa hazionyeshi kuwa amevaa sare za polisi au kufanya kitendo hicho kwenye kituo cha polisi, hivyo isitafsiriwe kuwa Jeshi la Polisi ndio limefanya."

Akizungumzia mikakati ya jeshi hilo katika kukomesha ushoga ndani ya Polisi Zanzibar, Kamishna Hamad aliwataka askari wote wenye mwenendo wa aina hiyo, wajisalimishe kwenye uongozi ili warekebishwe waendane na utamaduni wa jeshi hilo.

"Lengo sio kuwafukuza kazi, bali ni kuwarekebisha, kwa sababu huwezi kujua anafanya vitendo hivyo kwa sababu gani. Inawezekana alishafanyiwa kitendo hicho tokea utotoni na hawezi kujitetea na anaendelea kujizuru," alifafanua.

Kuhusu namna ya kuwatambua wenye tabia hiyo, alisema taratibu za polisi wakati wa kuajiri hazihusishi utambuzi wa tabia za ushoga kwa mwajiriwa bali hupimwa afya zao kwa ujumla.

Pia alisema Jeshi la Polisi lina taratibu na sheria zake ambazo zimeainisha makosa yote ambayo askari wa jeshi hilo hapaswi kufanya pamoja na hukumu zake endapo atafanya makosa hayo.

"Humu ndani ya kitabu hiki (sheria za polisi) kuna utaratibu mzima wa jeshi umewekwa. Kwa hivyo, askari anayefanya makosa ambayo yameainishwa humu ikiwamo hayo ya kufanya mapenzi ya jinsia moja, kuna mahakama za kijeshi na hukumu zimewekwa," alisema.




## CHADEMA yaahidi uraia pacha itakapoingia Ikulu

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimesema kikiingia madarakani, kitaweka utaratibu wa uraia pacha kwa kila Mtanzania atakayehitaji.

Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe alisema hayo wakati akizungumza katika mikutano tofauti akiwa mkoani Njombe juzi ikiwa ni mwendelezo wa mikutano ya hadhara ya chama hicho katika Kanda ya Nyasa.

Alisema nchi nyingi duniani zimeweka utaratibu wa wananchi wake kuwa na uraia pacha na kutokana na utaratibu huo umesaidia kuziongezea pato kwenye nchi zao.

"Na huo ni mtaji mkubwa wa kuongeza pato la taifa kwa sababu vijana wengi wanapata ajira, wakikosa katika nchi moja wanakwenda kupata katika nchi nyingine.

"Siku mkitupa serikali sisi CHADEMA, Watanzania wote wanaotaka uraia wa nchi yoyote, watapata. Wewe ukisoma hapa huna ajira, kama unaweza ukaenda Dubai ukapata kazi nenda na ukipata uraia sawa. Tutahakikisha vijana wote wanaokosa ajira kwenye nchi hii wanapata uwezo wa kwenda nchi nyingine kutafuta ajira."

Mbowe alisema idadi ya Watanzania wanaoishi nje ya nchi bado ni ndogo.

"Katika kila Mtanzania mmoja aliyeko nje, raia wa nchi nyingine ya Afrika Mashariki wako 20, serikali zao zinawapa uhuru. Msimamo wa CHADEMA ni kufika hapo, lakini tunasema ili kufika hapo ni lazima tulete mabadiliko makubwa ya Katiba.

"Tunataka kuhakikisha kwamba sisi kama chama kikubwa kazi yetu ya kwanza ni kupata Katiba mpya, ili viongozi wote wakatokane na chaguzi zilizo huru na haki," alisema.




Mkurugenzi wa Wateja Binafsi wa Benki ya CRDB, Bonaventure Paul (katikati), akipokea cheti cha tuzo ya benki bora inayohudumia wafanyabiashara wadogo na wa kati Tanzania 2023 kutoka kwa Mchapishaji na Mkurugenzi wa Uhariri wa Jarida maarufu la Global Finance, Joseph Giarraputo, jijini London, nchini Uingereza hivi karibuni. Kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Biashara wa benki hiyo, Toyi Ruvumbagu. **PICHA: MPIGAPICHA MAALUM**

# CRDB yatwaa tuzo ya benki bora utoaji huduma kwa wajasiriamali

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imetwaa tuzo ya Benki Bora inayohudumia wafanyabiashara wadogo na wa kati Tanzania inayotolewa na Jarida maarufu la Global Finance kwa mwaka 2023.

Hafla ya utoaji wa tuzo hizo ilifanyika hivi karibuni jijini London, Uingereza.

Jarida la Global Finance linawasaidia wakuu wa mashirika, benki na wawekezaji kubadilishana uzoefu kwenye masuala ya biashara na fedha na viwango vya jarida hilo vimeaminika kwa benki na washirika.

Benki zilizopata tuzo hiyo kwa mwaka huu zimechaguliwa kutoka miongoni mwa benki nyingi ulimwenguni kutoka kwenye mabara ya Afrika, Asia-Pacific, nchi za Caribbean, Ulaya Mashariki na Kati, Amerika ya Kusini, Mashariki ya Kati, Amerika ya Kaskazini na Ulaya Magharibi.

"Ni heshimu kubwa kwetu kupokea tuzo hii maalum ambayo ni ushuhuda wa wazi kwenye mchango wetu kwa biashara ndogo na za kati nchini Tanzania.

"Utendaji wetu kwenye sekta hii umetokana na mpango mkakati na ushirikiano ambao umetuwezesha kuendelea kukuza uwezo wetu katika utoaji wa huduma za kifedha," alisema Bonaventure Paul, Mkurugenzi wa Wateja Wadogo wa Benki ya CRDB.

Hivi karibuni, Benki ya CRDB ilipokea mkopo wa Euro milioni 150 kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) ambao utaongeza upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya biashara ndogo na za kati nchini, zikiwamo zinazomilikiwa na wanawake na kuwezesha uchumi wa bahari.

Mkopo wa EIB utasaidia kukuza biashara, kuleta usawa wa kijinsia na wanawezesha wanawake, pia kuziwezesha kampuni za uchumi wa bahari kuwekeza kwa maendeleo ya baadaye.

Benki ya CRDB imepewa tuzo hiyo kwa Tanzania kutokana na utafiti huru, ukihusisha wataalamu wa ndani ya sekta ya benki, viongozi waandamizi na wabobezi wa teknolojia kwa kutumia taaluma ya masoko na mahitaji, bidhaa na huduma, msimamo wa soko na ubunifu.

Tuzo hiyo inadhihirisha utayari wa Benki ya CRBD kuwezesha wateja wake kufanikiwa kwa kuhakikisha kwamba kila mmiliki wa kampuni ndogo na ya kati anapata usaidizi ili kufikia malengo yake ya mahitaji ya kibenki.

Tuzo za mwaka huu zimezingatia utendaji kwa kipindi cha kuanzia Aprili Mosi, 2021 hadi Machi 31, 2022.

Ni benki tano tu Afrika zimepewa tuzo hiyo, CRDB ikiwa ni benki pekee kutoka ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

TANGAZO KWA WADAIWA WA VIWANJA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia wananchi wote wanaodaiwa viwanja katika maeneo ya Mtumba, Michese, Nzuguni, Kitelela, Kikombo, Iyumbu, Nzuguni Bus Stand, Nala Industrial Area, Njedengwa Investment Area, Nala, Chahwa, Iyumbu New Town Centre, Mahomanyika, Vikonje, Nala Chigongwe, Ihumwa, Mapinduzi, Medeli, Nala Iugala, Nala Segu kukamilisha malipo ya viwanja hivyo mapema.

Mwananchi au taasisi itakayoshindwa kulipia kiwanja hadi kufikia tarehe 25 Machi, 2023 atambue kuwa kiwanja hicho kitauzwa kwa mteja mwingine ili kuboresha huduma katika Halmashauri bila kutoa taarifa yeyote kwa mteja wa awali.

**Tangazo hili limetolewa na:**

Joseph C. Mafuru
MKURUGENZI WA JIJI
DODOMA

MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA
S.L.P. 1249,
DODOMA

217303602

# WCF: Kuna ongezeko kubwa waajiri wapya

**Na Waandishi Wetu,** DODOMA

KUMEKUWA na ongezeko kubwa la waajiri kujisajili na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) katika kipindi cha uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma amesema.

Katika mkutano na waandishi wa habari jana jijini hapa, Dk. Mduma alibainisha kuwa katika kipindi cha kuanzia Machi 2021 hadi Februari mwaka huu, waajiri wapya 5,250 wamejisajili WCF.

Alisema kwa taarifa zisizokaguliwa hadi kufikia Februari mwaka huu, WCF ilikuwa imesajili jumla ya waajiri 29,978. Kati yao, asilimia 99.27 ni waajiri wakubwa, huku asilimia 98.71 ni waajiri wa kati na waajiri wa chini ni asilimia 88.56.

"Hatua za makusudi za serikali chini ya uongozi wa Rais Samia za kuweka vivutio vya kufanya biashara na kuondoa vikwazo vilivyokuwapo ikiwa ni pamoja na kupunguza viwango vya uchangiaji na kutoa msamaha wa riba, vimechangia ongezeko hilo," alisisitiza Dk. Mduma.

Alisema kwa sasa mwajiri amepunguziwa mzigo wa kuchangia kwenye mfuko ambapo serikali ilipunguza kiwango cha mchango kwa Sekta Binafsi kutoka asilimia moja ya awali kabla ya maboresho ya kisera hadi asilimia 0.5 ya sasa na hivyo kuleta ulinganifu wa michango kuwa sawa na Sekta ya Umma.

**ULIPAJI WA MAFAO**

Alibainisha kuwa kabla ya kuanzishwa kwa WCF, malipo ya fidia nchini kwa mwaka mzima yalikuwa chini ya Sh. milioni 200 lakini baada ya kuanzishwa kwa WCF, malipo yanaongezeka mwaka hadi mwaka.

"Takwimu za hivi karibuni zinaonyesha toka kuanzishwa kwa mfuko, idadi ya wanufaika wa mfuko imefikia 10,454 ambao wamelipwa jumla ya Sh. bilioni 49.44," alibainisha.

Akifafanua kuhusu mafao, mkurugenzi huyo alisema kuna mafao ya aina mbalimbali ambayo mfuko unatoa ikiwa ni pamoja na huduma ya matibabu, malipo ya ulemavu wa muda, malipo ya ulemavu wa kudumu yanayotolewa kwa mfumo wa pensheni ya kila mwezi, malipo kwa anayemhudumia mgonjwa (mfanyakazi), huduma za utengamao, msaada wa mazishi na malipo kwa wategemezi endapo mfanyakazi atafariki dunia.

**FIDIA MTANDAONI**

Dk. Mduma alisema mfuko umeendelea kusogeza huduma karibu na wadau wake na sasa huduma zote muhimu zinapatikana nchi nzima kwa njia ya mtandao.

Alizitaja huduma hizo kuwa ni pamoja na usajili wa wanachama ambapo mwanachama wa mfuko huu ni waajiri, kupata cheti cha usajili, kuwasilisha michango ya kila mwezi, mfuko unapokea michango kupitia nambari ya udhibiti (control number) ambayo hupatikana kwa njia ya mtandao.

Huduma zingine ni kuwasilisha taarifa za michango, kufanya mabadiliko ya taarifa za wafanyakazi wao, kuwasilisha taarifa ya ajali, ugonjwa au kifo cha mfanyakazi kilichotokana na kazi na kufuatilia mwenendo wa madai.

Dk. Mduma aliwakumbusha waajiri wote kuwa kwa mujibu wa sheria, mwajiri ndiye mwenye jukumu la kuchangia kwenye mfuko na ni kosa la jinai kwa mwajiri kumkata mshahara mfanyakazi wake kwa ajili ya kuchangia WCF.

Alisisitiza kupungua kwa kiwango cha uchangiaji hakutaathiri utoaji wa mafao kwani mfuko umeshirikiana na wataalamu wa uhimilivu na kujihakikishia WCF itakuwa endelevu.

HABARI KITAIFA

# CCM yafungua mafaili ya wanaojipitisha majimboni

**Na Augusta Njoji,** IRAMBA

CHAMA Cha Mapinduzi(CCM) kimefungua mafaili ya kukusanya taarifa za wanachama wanaokiuka maadili ikiwamo kujipitisha kwenye majimbo na kata kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

Vilevile, kimetoa onyo kwa makatibu wa CCM kuanzia shina hadi mikoa watakaobainika kutowatenda haki wanachama na wanaoendekeza ulevi.

Akizungumza na wanachama wa CCM na wananchi wa Wilaya ya Iramba mkoani Singida jana, Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, alisema kwa sasa ni wakati wa kufanya kazi kwa kushikamana na kuacha chokochoko.

"Wakati wa kufanya kazi tushikamane, tuache chokochoko. Mbunge wa jimbo hili yupo na majimbo yote ya chama chetu sitegemei kumwona mtu anaanza kujipitisha, hapana! Vivyo hivyo kwa viti maalum, acheni watu wafanye kazi, subiri muda mwafaka. "Sisi tumefungua mafaili, niwaambie si mmeona utaratibu wa mwaka jana kwenye chama mambo yalikuwaje, huyu kata, huyu kata, wanasoma sifa na matatizo yake, ninasema kata huyu, jamaa mlevi wa kupindukia, ninasema kata.

"Ushahidi upo? Ndio, ninasema kata, juzi amekutwa baa yupo hoi taabani wamembeba wamempeleka kwake. Hivi tunataka viongozi wa aina hiyo? Sasa kama kiongozi mwenye dhamana kubwa ndani ya chama kazi yangu nini? Kata, sitegemei kuona mtu anatembea kibunge au kidiwani kabla ya 2025, acheni watu wafanye kazi," alionya.

Alisema chama kimekamilisha kutengeneza safu ya uongozi kwa kipindi cha miaka mitano na uchaguzi umeisha, hivyo hategemei kuona nongwa.

"Katibu yeyote wa CCM kuanzia shina hadi mkoa tukisikia unakuwa wa kwanza kwenye viti virefu, hufai tukisikia una tabia ya kwenda kukopa kila nyumba, hufai kuwa kiongozi. Tukisikia hutendi haki, hufai kuwa kiongozi, tunataka kiongozi anayesimamia taratibu ambaye hafanyi mambo yanayokwenda kinyume cha taratibu," alisisitiza.

Akiwa wilayani Mkalama, Chongolo alisema sifa ya kiongozi wa CCM ni kuzungumzia matatizo ya wananchi na kuyatafutia ufumbuzi.

"CCM imepewa dhamana ya kuongoza nchi, hatuji kupiga porojo, sisi tunakuja kusikiliza wananchi na kuchukua changamoto zao na kuzitatua," alisema.

Chongolo alisema CCM haiwezi kufanya kazi ya kupiga kelele bali inahangaika na mambo ya wananchi.

"Kuna wengine wanakuja wanasema hakuna kilichofanyika, hebu angalieni tangu uhuru hadi sasa maendeleo yaliyofanyika kwenye sekta ya elimu, afya, miundombinu, kila nyanja imeguswa kwa maendeleo," alisema.

Chongolo yupo mkoani Singida na sekretarieti yake kwa ziara ya kikazi kukagua utekelezaji wa Ilani ya CCM na kusikiliza kero za wananchi.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Mohamed Moyo (mwenye kofia), akiwa na viongozi mbalimbali, wakitoka kukagua madarasa yaliyochakaa ya Shule ya Msingi Majogo wilayani humo juzi. Moyo ameagiza kubomolewa kwa madarasa hayo, ili yajengwe upya kabla ya kuleta madhara kwa wanafunzi na walimu. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mwinyi ataka kipaumbele kwenye magonjwa adimu

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, ameagiza taasisi za serikali kutengeneza sera zitakazotoa uhakika wa matibabu bila kikwazo kwa watoto wanaougua magonjwa adimu.

Dk. Mwinyi alitoa kauli hiyo juzi jioni wakati wa maadhimisho ya siku ya magonjwa adimu yaliyofanyika katika Hospitali ya Aga Khan jijini Dar es Salaam, kwa kuwasha taa kama ishara ya kuitambua siku hiyo.

"Mimi na serikali yangu nataka niseme kwamba kwanza suala hili tunalitambua na tutafanya kila litakalowezekana kutoa mchango wetu katika kushughulikia watoto walioathirika na magonjwa haya," alisema Rais Mwinyi.

"Nadhani sasa hivi kinachotakiwa ni kuendelea kutoa elimu kwa umma ili utambue kwamba kuna watoto walioathirika na ugonjwa huo na wanahitaji msaada kwa maisha yao yote, lakini nazitaka taasisi za umma kutambua kuwapo kwa ugonjwa huo na kutengeneza sera za kuutambua."

"Sera hizo ziendane na ziwasaidie waathirika wa ugonjwa huo. Kama kiongozi wa serikali, mimi mwenyewe nitakuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba serikali inaweka sera nzuri madhubuti ambazo zitatoa kila aina ya msaada kwa ajili ya watoto hawa. Tunataka tutoe huduma hiyo bila malipo."

Daktari wa watoto wa Hospitali ya Aga Khan, Mariam Nuran, alisema ugonjwa huo huwapata wagonjwa wachache na hutokana na kurithi kutoka kwenye vinasaba.

"Huu ni ugonjwa unatokea kwa watoto wachache sana na ndio maana inaleta changamoto hata kupata tiba kamilifu. Magonjwa haya yanarithishwa kwenye vinasaba kwa hiyo yanahitaji tiba endelevu, ikiwamo ya mazoezi kuhakikisha viungo visikakamae au kuongezewa damu mara kwa mara," alisema Dk. Mariam.

Sarah Chande alisema amewahi kuishi na mtoto mwenye ugonjwa huo na gharama ya matibabu kwa magonjwa hayo ni kubwa pamoja na huduma za kila siku ambazo huhitajika.

"Kuwauguza hawa wagonjwa siyo kazi rahisi hata kidogo ni gharama kubwa ambayo kwa mwenye kipato kidogo ni vigumu kumudu na familia pia huwa hazielewi na wakati mwingine zinawaza vitu vingine ambavyo havipo, mtu anawaza ni ushirikina kwa hiyo usipokuwa makini unaweza kutumbukia huko.

"Badala ya kumsaidia mtoto unaweza kufupisha maisha yake, kwa hiyo ni vema tutambue kwamba haya magonjwa yapo na yanawaathiri sana watoto, tunaomba serikali itambue na itoe elimu kuhusu hayo magonjwa, najua wako wengine hawajitokezi kwa kuogopa fikra potofu.

Aliomba serikali kuweka kitengo maalumu cha kuwatambua watoto wenye ugonjwa huo kama ilivyo kwa magonjwa ya saratani na selimundu.

# Rwambow apendekeza upelelezi kuimarishwa

**Na Maulid Mmbaga**

KAMISHNA Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi mstaafu Jamal Rwambow, ameiomba serikali kukiwezesha kitengo cha upelelezi kwa kuwajengea uwezo wapelelezi ili watende kazi kwa ufanisi na kuondoa au kupunguza malalamiko.

Aidha, kwa uzoefu wake katika jeshi hilo alibaini baadhi ya askari wa kitengo cha upelelezi hawana uwezo mkubwa, huku kukiwa na bajeti ndogo kuwezesha uwapo wa vifaa na mahitaji mengine muhimu.

Alitoa ombi hilo jana baada ya kubainisha kuwa kuna baadhi ya wapelelezi wanasimamia na kuongoza shughuli za upelelezi wakati hawana taaluma kubwa ya masuala hayo.

Kamishna mstaafu Rwambow, ni mtaalamu wa masuala ya upelelezi na alihitimu stashahada ya upelelezi nchini Ujerumani mwaka 1985, pia alihitimu Astashahada ya sheria katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) mwaka 1977, na alitumikia Jeshi la Polisi kwa miaka 39.

Akizungumza na wanafunzi wa kozi ya uofisa katika Chuo cha Taaluma ya Polisi (DPA) mkoani Dar es Salaam, alisema shughuli ya upelelezi msingi wake mkubwa wa mafanikio unatokana na taarifa inayotoka kwa siri.

"Kupata taarifa ni gharana na bahati mbaya serikali haitoi bajeti ya kutosha kuwawezesha hawa watu kufanya kazi zao, Jeshi la Polisi kama lilivyo linauwezo mkubwa wa kufanya mambo mengi wao wenyewe," alisema Rwambow.

Kamishina wa Opereshi na Mafunzo ya Jeshi la Polisi nchini CP Awadhi Haji, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuliwezesha jeshi hilo kupata bajeti ya mafunzo yanayoendelea katika vyuo mbalimbali vya polisi nchini.

"Huko nyuma mafunzo haya katika vyuo vyetu wanafunzi walikuwa wakijigharamikia kwa kukatwa fedha inayotokana na posho ya chakula, lakini Rais Samia kwa kutambua umuhimu wa vyombo vyake aliona ni vizuri kuondosha hicho kilichokuwa kinafanyika na hatimaye sasa tunashiriki bila kuchangia kitu chochote," alisema Haji.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kufanyisha kazi wagonjwa ni ukiukwaji haki za binadamu

**MALALAMIKO** kwamba kuna baadhi ya watumishi wa Idara ya Afya mkoani Rukwa wenye tabia ya kuwafanyisha kazi wagonjwa kabla ya kuwapatia huduma ni unyanyasaji na ukiukwaji wa haki za binadamu.

Mgonjwa anapokwenda hospitali maana yake afya yake imetetereka hivyo anahitaji matibabu ili iweze kutengemaa.

Mgonjwa huyo ambaye amekwenda kupata huduma ya matibabu na badala yake anapewa jembe kupalilia majani au ufagio kusafisha uwanja, ni kitendo cha kinyama na kinapaswa kukemewa kwa nguvu zote.

Katika hali ya kawaida, mtu mwenye akili timamu hawezi kumtumikisha mgonjwa ambaye ni dhaifu kutokana na afya yake kutokuwa vizuri.

Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Queen Sendiga, alilalamikiwa kuhusu tabia hiyo na baadhi ya wananchi alipokwenda kutembelea zahanati katika Kijiji cha Nambogo, Manispaa ya Sumbawanga.

Mmoja wa wananchi hao alimlalamikia mkuu huyo wa mkoa kuwa katika zahanati hiyo kumekuwa na mtindo mgonjwa apokwenda kupata matibabu, kwanza anapewa vifaa vya kufanyia usafi na kupewa eneo asafishe akimaliza ndipo anapata matibabu.

"Mkuu wa mkoa sisi tunashangaa hapa hospitali yetu tunakuja na mgonjwa au anakuja mtu ni mgonjwa akifika anapewa jembe apalie na kufanya usafi maeneo ya hospitali akimaliza ndipo anapewa huduma ya matibabu."

Hatua iliyochukuliwa na Mkuu wa Mkoa ni kumwagiza ofisa utumishi kuwaondoa watumishi hao katika kituo hicho.

Sisi tunasema pamoja na Mkuu wa Mkoa kuagiza hatua hiyo ichukuliwe, lakini watumishi hao wanapaswa kupewa adhabu kali ambayo itawafanya wajutie kitendo chao.

Kama wagonjwa hao wangekuwa ndugu wa watumishi hao wangethubutu kuwapa kazi hiyo ya kusafisha mazingira?

Ndio maana tunasema huo ni ukiukwaji wa haki za binadamu kwa sababu kila mtu anastahili kupata haki yake ya kuishi na kuwa na afya bora.

Kinachoshangaza hata Mganga Mkuu alikiri kupata malalamiko, lakini hakuna hatua iliyochukuliwa mpaka Mkuu wa Mkoa alipofika na kupata malalamiko hayo kutoka kwa wananchi.

Tabia hii ya kulea watu wanaoitia doa Idara ya Afya na kuonekana sehemu ambayo haitendi haki kwa wateja wake, lazima ikomeshwe ili kurudisha imani kwa wananchi.

Watu wachache ndio wanaotia doa kazi nzuri inayofanywa na wengine kwa moyo wa kijitoa na kuwakatisha tamaa kutokana na shutuma zinazotolewa.

Kama alivyoahidi Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga kuwa tayari amekwisha anza kuchukua hatua kwa kufanya uchunguzi ni vizuri ukafanyika kwa haraka ili wahusika waadhibiwe ipasavyo.

Watu wachache wasiharibu nia nzuri ya serikali ya kuwapatia wananchi wake huduma bora za matibabu kwa kuweka mazingira mazuri ya wagonjwa kupata huduma nzuri.

Ni vizuri pia katika maeneo yanayotoa huduma za jamii kuwapo na masanduku ya kutoa maoni ili kama kuna kero yoyote wananchi waweze kuwasilisha kwa njia ya maandishi kama uwezekano wa kuonana na viongozi unakuwa mgumu.

Nia njema ya Rais Samia Hassan ya kuboresha huduma katika sekta ya afya isiharibiwe na watu wachache na kama alivyosema mkuu wa mkoa kuwa kamwe yeye binafsi hatawavumilia watu hao katika mkoa wa Rukwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ujue undani ulioko maisha ya makondakta na madereva wao

Na Halfani Chusi

**HAWA** jamaa ni marafiki sana. Huwa wanataniana, lakini kila mmoja anayafahamu mapungufu ya mwenzake. Ni rahisi kugombana hata kutofautiana kwa maneno, lakini si rahisi ugomvi wao kudumu kwa zaidi ya dakika 30.

Hii ni kwa sababu, dereva muda wote huwa anahisi kondakta wake anampiga kwenye masuala ya fedha, kwa sababu kondakta ndiye mshika hazina.

Lakini, kondakta mara nyingi ndio huwa anaenda kupaki gari wakati wa kulaza na asubuhi dereva ndio huwa anaamsha, kwa sababu ya maandalizi ya kuingia barabarani kusaka riziki.

Hii ni kwa sababu dereva huwa anaamini, kondakta wake hayupo vizuri kwenye udereva kama alivyo yeye. Ndio maana, humpa gari akalipaki likiwa halina abiria na kwa sababu yeye ndio huwa anatambulika kwa bosi, kwa hiyo anakuwa na mamlaka zaidi.

Akiamini huo ndio muda sahihi kwake kujifunza gari au kukomaza ujuzi wake, makondakta wengi ambao sasa ni madereva, wamepitia hatua hiyo.

Usishangae kuona kondakta akatumia muda huo mdogo, kuimarika na kuendesha gari, kwa sababu akishajua kama hajakomaa vizuri kwenye udereva, huwa anaongeza umakini kumuangalia dereva wake, akiamini nafasi yake ni cheo kidogo.

Ni vigumu sana kufahamu undani wa maisha yao, mpaka pale ufanye uchunguzi wa kina kama Nipashe ilivyothubutu ili hali muda wote sura zao huwa zimetawaliwa na furaha.

**Ni vigumu sana kufahamu undani wa maisha yao, mpaka pale ufanye uchunguzi wa kina kama Nipashe ilivyothubutu. ili hali muda wote sura zao huwa zimetawaliwa na furaha.**

Kwenye maisha yao, kondakta ndio mwenye jukumu la kuita na kushawishi abiria, lakini cha ajabu kondakta akificha hata shilingi 2,000, dereva anajua na ndoa zao mara nyingi huvunjikia hapo.

Unaweza kujiuliza anawezaje kujua? Jibu ni kwamba, dereva ana uwezo mkubwa wa kukariri wingi wa watu kwenye gari na kujua kwa wingi huo, kinaweza kupatikana kiasi fulani na ikawa kweli. Pia, hatua ya kukariri vituo ambavyo abiria wamepanda na kushuka.

Kuna muda, ugomvi hutokea kati yao pale dereva anapotumia pesa nyingi kwa kula vitu vya kupita kama vile karanga, maji, juisi, na kumpa maelekezo muuzaji 'kachukue fedha kwa kondakta'. Hilo kuna muda linaibua utata kwenye kugawana mapato wakati wa kufunga siku kibiashara.

Mara nyingi dereva, huwa si rahisi kukumbuka alichokula njiani, kwa sababu kwanza yeye sio mlipaji na muda mrefu anakuwa 'bize' kuangalia abiria na mwenendo mzima wa siku hiyo.

Lakini hao jamaa, hawawezi kuwa tofauti hata siku moja inapotokea wamesababisha ajali. Hapo wanaungana na kuwa kitu kimoja, kutetea masilahi yao kwa kuwa ikitokea wameshindwa kulikabili, hilo wote litawagharimu kwa bosi wao.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe, ukabaini wawili hao wana tabia za kujali familia kuliko kawaida, kama ambavyo mara nyingi hujinasibu kwa kusema "bora nishuke bila hela, lakini 'mazaga' yapatikane familia ile."

Japo hawana tabia ya kutunza fedha, kondakta au dereva anaweza kuwa kwenye chombo cha moto siku zote, lakini akiachishwa kazi siku moja tu na pesa imeisha hapohapo.

Hiyo inatokana na asili ya kazi yao, huwa wanakuwa wagumu kuweka bajeti kwa kuwa kazi yao ni ya kuingiza kila siku kwa hiyo wengi wao huweka dhana ya nitapata tena kesho.

**0787879707**

# Mpango mafunzo teknolojia magari, mitambo ya China wazinduliwa NIT

**Na Prosper Makene**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) na Taasisi ya Ufundi ya Zibo (ZBVI) ya China wamezindua mafunzo ya pamoja kwa wanafunzi wa uhandisi wa magari (Automobile Engineering) wa NIT kufundishwa teknolojia za magari ya kichina na mitambo.

Kundi la kwanza la wanafunzi 39 wa NIT litaanza kunufaika na mpango huo, wakianza kufundishwa teknolojia za magari na mitambo ya kichina kuanzia mwaka huu wa masomo, 2022/23.

Programu hiyo ya mafunzo imeanzishwa baada ya juhudi za pamoja zilizofanywa na vyuo vya NIT, ZBVI na Taasisi ya Mafunzo ya Mafuta na Gesi ya Sunmaker.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa awamu ya kwanza ya mafunzo kwa wanafunzi wa uhandisi wa magari uliofanyika kupitia Zoom, Mkuu wa NIT, Prof. Zacharia Mganilwa, alisema jana kuwa wanafunzi hao wanaanza kufundishwa lugha ya kichina kabla ya kuendelea na mpango mzima wa kufundishwa teknolojia mbalimbali za magari na mitambo ya kichina.

"Tumezindua leo batch (awamu) ya kwanza ya wanafunzi ambao watapata mafunzo maalum ya teknolojia ya magari na mitambo ya kichina. Wanafunzi hawa baada ya kuhitimu masomo yao watakuwa na uwezo mkubwa wa kufanya matengenezo mitambo na magari mbalimbali yanayotengenezwa China," alisema.

Mkuu huyo alidokeza kuwa mafunzo hayo maalum yatapanua wigo wa maarifa kwa wanafunzi watakaobahatika kusoma kozi hiyo kwa kuwa pia watatumia lugha ya kichina ambayo watafundishwa katika shughuli zao za kibiashara baada ya kuhitimu.

Aliendelea kusema kuwa wanafunzi watakaohitimu katika programu, watakuwa wabobezi katika utambuzi na ukarabati wa mifumo ya umeme na mitambo ya magari ya kichina, pia watakuwa mahiri katika utambuzi na ukarabati wa mifumo ya kielektroniki wa magari hayo.

Prof. Mganilwa alitaja ujuzi mwingine ambao mhitimu wa kozi hiyo maalumu atakuwa nao baada ya kuhitimu ni pamoja na kuwa na uwezo wa kina wa utambuzi na ukarabati wa magari.

"Programu hii itafanyika kwa muda usiozidi miaka minne, mihula miwili kwa mwaka na katika kila muhula, wanafunzi watafundishwa angalau moduli moja," Prof. Mganilwa alisema.

Aliongeza kuwa wameweka mpango wa mafunzo kwa muda huo ili kuwasaidia wanafunzi kuelewa kwa kina soko la sasa la magari na mitambo inayotengenezwa China.

Mkuu wa Chuo cha ZBVI, Prof. Sun Qiyou alisema kuwa katika mpango huo, chuo chao kitatoa wataalamu wa mafunzo hayo ya ufundi stadi.

Prof. Qiyou aliongeza kuwa kulingana na mpango huo, hatua ya kwanza kwa wanafunzi wa NIT waliobahatika kusoma kozi hiyo, wataanza kujifunza lugha ya Kichina na baada ya hapo watafundishwa kozi hiyo ya ufundi stadi kwenye maeneo ya ufundi wa magari na mitambo.

Alisema kwa sasa kutokana na mwingiliano wa kiuchumi na kiutamaduni kati ya China na Tanzania ambao unazidi kuimarika, Serikali ya China inaendelea kuunga mkono Tanzania katika kuimarisha ushirikiano hususani katika eneo hili la elimu.

"Tunatumaini kwamba wanafunzi wanaoshiriki katika mafunzo hayo watathamini fursa hii na kujifunza kwa ufanisi. Ninaamini kwamba kwa ushirikiano wa dhati wa pande zote, mradi utakwenda vizuri na kufikia matokeo yaliyotarajiwa," alisema.

Mwalimu wa lugha ya Kichina, Bi. An Qi alisema matarajio ya kwanza ni kuona wanafunzi wote waliopata bahati ya kusoma kozi hiyo wanafahamu vyema lugha hiyo.

"Ninaamini kuwa kwa juhudi zetu za pamoja, mradi huu utakuwa na matokeo mazuri sana, utawasaidia wanafunzi hawa kujifunza kwa kina teknolojia mbalimbali za magari na mitambo ya kichina kwa lugha ya Kichina," alisema.

Akizungumza hafla hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Sunmaker, Dk. Felix Duan, alisema: "Tunatumaini kuwa wanafunzi waliochaguliwa watajifunza na kupata ujuzi zaidi katika teknolojia za kichina."

Akizungumza kwa niaba ya walionufaika na mradi huo, mwanafunzi wa NIT anayesomea ufundi wa magari, Joseph Odhiambo alisema: "Kwa niaba ya wanafunzi wote tulionufaika na mpango huu, tunakishukuru chuo chetu pamoja na taasisi ya ufundi ya ZIBO na Kampuni ya Sunmaker kwa kutupatia fursa hii adhimu ambayo itatusaidia kusoma na kujifunza teknolojia za magari na mitambo mbalimbali ya kichina. "Tunawaahidi kuwa tutajifunza kwa bidii kozi hii ambayo itatuwezesha vilevile kujifunza lugha ya Kichina pamoja tamaduni za Wachina. Tuna imani kuwa kozi hii itatuwezesha kwa kiasi kikubwa kufanya kazi kimataifa hususani katika teknolojia za matengenezo kwenye karakana za magari na mitambo ya kichina duniani."


TRA

## MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

**Imethibitishwa na ISO 9001: 2015**

## TAARIFA KWA UMMA

### Kusudio la Kufuta Usajili wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Wafanyabiashara Wasio na Sifa za Kuendelea Kusajiliwa katika VAT

**Dar es Salaam, 01 Machi, 2023:**

Kwa mujibu wa **Kifungu 28** na **29 cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148 (Rekebisho la Mwaka 2019),** wafanyabiashara waliotimiza vigezo vya kusajiliwa katika Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), wanatakiwa kuomba usajili huo kwa Kamishna Mkuu. Moja ya vigezo vya kusajiliwa katika VAT ni kuwa na mauzo kwa mwaka, yanayozidi kiwango cha chini kilichowekwa na **Kanuni ya 14 ya Kanuni za VAT za mwaka 2015** cha **Shilingi Milioni Mia Moja.**

Tathmini iliyofanyika kupitia kumbukumbu zetu za usajili wa VAT imebainisha kuwa, baadhi ya walipakodi waliosajiliwa katika VAT, wamepoteza sifa za kuendelea kuwa katika usajili ikiwa ni pamoja na biashara zao kutofikisha mauzo ya milioni mia moja kwa mwaka. Ili kuimarisha usimamizi mzuri katika VAT, Kamishna Mkuu anakusudia kutumia mamlaka aliyokasimiwa chini ya **Kifungu cha 41 cha Sheria ya VAT**, kuwafutia usajili walipakodi wote wenye mauzo chini ya kiwango tajwa, pamoja na wale waliopoteza sifa zilizoainishwa chini ya **Kifungu cha 29 cha Sheria ya VAT. Hata hivyo, kusudio hili halilengi kumuondolea mlipakodi wajibu wake wa kulipa kodi au kuwasilisha ritani za kodi za kipindi cha nyuma kwa walipakodi wanaotarajiwa kufutiwa usajili wa VAT.**

Kutokana na ufafanuzi huu, tunawajulisha kuwa **orodha kamili ya majina ya walipakodi wanaotarajiwa kufutiwa usajili wa VAT imewekwa kwenye tovuti ya TRA (www.tra.go.tz).** Mlipakodi yeyote mwenye pingamizi juu ya maamuzi ya Kamishna Mkuu, anatakiwa kuwasilisha pingamizi lake, akielezea sababu za kwanini asifutiwe usajiliwa VAT. Pingamizi ziwasilishwe katika **Ofisi za TRA kwa Meneja wa Mkoa husika** na **ziwasilishwe ndani ya siku thelathini (30) kuanzia tarehe ya notisi hii.** Baada ya siku 30 zilizowekwa kupita, Mamlaka itaendelea na zoezi la kufuta usajili wa VAT.

Kwa taarifa zaidi, tembelea ofisi za TRA zilizo karibu nawe au tumia mawasiliano yafuatayo

| | |
|---|---|
| **Tovuti:** | www.tra.go.tz |
| **Namba ya Bure:** | 0800 750 075 au 0800 780 078 |
| **WhatsApp:** | 0744 23 33 33 |
| **Barua Pepe:** | huduma@tra.go.tz au services@tra.go.tz |

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

A.J. Kidata
Kamishna Mkuu




Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa Benki ya Stanbic Tanzania, Omari Mtiga (kulia) na Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja, Ester Manase (wa pili kulia), wakikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni tano kwa Lucia Tarama Minde jijini Dar es Salaam juzi, baada ya kuibuka mshindi wa kampeni ya benki hiyo ya "Mchongo ni Kuchanja na Stanbic Visa" iliyoundwa kwa ajili ya kuwazawadia wateja wanaotumia kadi ya Stanbic Visa kwenye mashine za kulipa za kielektroniki wanapofanya manunuzi na huduma. **PICHA: MARY GEOFREY**

# 78 wanaodaiwa kufanya udanganyifu NHIF wakabidhiwa Tume ya Walimu

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

MAJINA 78 ya walimu wanaodaiwa kughushi nyaraka mbalimbali za wategemezi wao pamoja na matumizi mabaya ya kadi za matibabu kwa lengo la kutaka kusajiliwa katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), yamekabidhiwa kwa Tume ya Utumishi wa Walimu kwa hatua zaidi.

Walimu hao wanadaiwa kughushi nyaraka za vyeti vya kuzaliwa na vya ndoa, wakitaka kuthibitisha uhusiano wa kuwapo kwenye ndoa ili wapate huduma zinazotolewa na mfuko huo.

Makabidhiano ya majina hayo yalifanyika juzi makao Makuu ya NHIF jijini Dodoma wakati wa kikao kati ya Menejimenti ya Mfuko huo na ya Tume ya Utumishi wa Walimu, kupitia ripoti inayoonyesha namna udanganyifu huo ulivyofanyika na hasara waliyoisababisha kwenye mfuko huo.

Mkurugenzi wa NHIF, Bernard Konga alisema tayari wameshachukua hatua mbalimbali kwa watuhumiwa hao ambao walikiri kutenda makosa hayo, ikiwamo kuwafungulia kesi, kuwafungia matumizi ya kadi na kuwataka kurejesha fedha zilizotumika kuwahudumia wategemezi wao visivyo halali.

"Tunachukua hatua nyingi kwa watuhumiwa wa udanganyifu na mpaka sasa kuna kesi zinaendelea katika mikoa ya Geita, Dodoma na Dar es Salaam, kadi za matibabu za watuhumiwa hao zimefungiwa na kuwaandikia barua za onyo," alisema Konga.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Paulina Nkwama alisema vitendo vilivyofanywa na walimu hao ni ukiukwaji wa maadili ya utumishi wa umma na havikubaliki, hivyo watachukua hatua.

Pia alisema watashirikiana na NHIF kupambana na wimbi hilo la udanganyifu unaofanywa na baadhi ya walimu pamoja na kuelimisha madhara ya kughushi au kufanya udanganyifu wowote kupitia kadi ya matibabu.

Akiwasilisha taarifa ya uchunguzi wa udanganyifu uliofanywa na watumishi wa umma, Meneja wa Kitengo cha Kupambana na Udanganyifu cha NHIF, Dk. Rose Ntundu alisema kuwa kati ya watumishi wa umma 99 waliobainika kufanya udanganyifu, 78 ni wa shule za serikali za msingi na sekondari.

# GGML yashinda tuzo ya kimataifa usalama kwa mwaka wa 4 mfululizo

**Na Mwandishi Wetu**

MISINGI imara ya udhibiti wa hali ya usalama katika utendaji kazi ndani na nje ya Mgodi wa Geita Gold Mining Limited (GGML) imeendelea kuifanya kampuni hiyo kuandika historia duniani baada ya kushinda kwa mara ya nne mfululizo tuzo ya kimataifa ya usalama mahala pa kazi (Global Safety Award).

Katika tuzo hiyo inayotolewa na kundi la kampuni za AngloGold Ashanti (AGA), GGML ilishinda mwaka 2019, 2020, 2021 na wiki hii imeshinda tuzo hiyo kwa mwaka 2022.

Akizungumzia ushindi huo katika mahojiano mkoani Geita jana, Meneja Mwandamizi wa Afya, Usalama, Mazingira na Mafunzo wa GGML, Dk. Kiva Mvungi alisema tuzo hiyo inamaanisha kuwa AGA imeitambua GGML kama kampuni kinara inayofanya vizuri katika masuala ya usalama duniani.

AGA ambayo imeorodheshwa kwenye masoko ya hisa ya Johannesburg, New York, Australia na Ghana inamiliki migodi katika nchi za Australia, Columbia, Argentina, Brazil, Ghana na Tanzania. Katika nchi zote hizo, GGML au Watanzania kwa ujumla ndio vinara wa kuzingatia masuala ya usalama mahala pa kazi.

Dk. Kiva Mvungi alisema mafanikio hayo hayakuja kirahisi kwa kuwa GGML imefanikiwa kuimarisha ushirikiano wa wafanyakazi ambao wamekuwa wakiuonesha katika kujali afya zao pamoja na kujali usalama kazini. Alisema kitu ambacho wamefanya tofauti na wenzao ni kwamba walibadilisha mfumo wa mawasiliano ya kiusalama, badala ya kutoka kwa viongozi kwenda kwa wafanyakazi, waliweka utaratibu kwamba mfumo huo wa mawasiliano utoke kwa wafanyakazi kuja kwa viongozi.

Akizungumza ushindi huo wa tuzo nne mfululizo, Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Terry Strong aliipongeza timu nzima ya idara ya afya, usalama na mazingira pamoja na wafanyakazi wote wa GGML kwa kudumisha usalama wao ndani na nje ya kampuni.

Mbali na tuzo hiyo ya kimataifa ya usalama, anasema GGML pia ilipata tuzo ya utendaji bora wa jumla.

"Hakika tuzo hii inaonyesha namna tunavyofanya vizuri na kuthaminiwa. Juhudi zenu zinatambuliwa vyema na kampuni nzima. Kama tunavyojua sote bado tuna changamoto nyingi za kufanyia kazi kama timu lakini nina uhakika tunaweza kufanya kazi pamoja na kutimiza yote tuliyojiwekea Kongole kwenu wote," alisema mkurugenzi huyo.

Mmoja wa wafanyakazi wa idara hiyo ya usalama, afya na mazingira ndani ya GGML, Dk. Subira Joseph ambaye amefanya kazi ndani ya kampuni hiyo kwa zaidi ya miaka 10 kama daktari kwenye kituo cha afya cha GGML pamoja na Josephine Kimambo ambaye ni Mhandisi wa Mazingira, walisema ushindi mfululizo wa tuzo hiyo umewafanya waone wanafanya kazi kwenye mazingira salama.

# Uswisi yaahidi kuipaisha Tanzania katika biashara

**Na Halfani Chusi**

KILIO cha wafanyabiashara nchini, kukosa soko la kuuza bidhaa zao Uswisi, kimefikia ukomo baada ya Uswisi kuzindua chemba ya wafanyabiashara kati yake na Tanzania yenye lengo la kuwaunganisha na kufanya biashara pamoja.

Akizungumza kwenye uzinduzi huo uliofanyika juzi Dar es Salaam, Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema hatua hiyo itarahisisha ufanyaji wa biashara kati ya nchi ya Tanzania na Uswisi pamoja na kuongeza ajira kwa vijana.

Pia alisema kitendo hicho kitaleta manufaa makubwa nchini ikiwamo kuinua uchumi wa nchi, kutanua wigo wa biashara pamoja na kuongeza mianya ya upatikanaji fedha kwa wafanyabiashara.

"Ni fursa nzuri na adhimu kwa Watanzania, kwa sababu chemba hii itatuletea manufaa makubwa, kutusaidia kujua namna ya kuzalisha bidhaa zenye ubora kama ilivyo kwa wao, hali itakayowafanya wawekezaji wengine kujua Tanzania tuna uwezo wa kuzalisha bidhaa shindani duniani.

"Pia itasaidia kuimarisha ushirikiano na uhusiano mzuri kwenye maeneo ya uchumi, uwekezaji, viwanda, biashara na elimu baina ya nchi hizi mbili," alisema Kigahe.

Kiongozi huyo alifafanua kuwa serikali imewekeza nguvu kwenye uwekezaji wa biashara, akisisitiza kuwa uzinduzi huo utaisaidia kuipeleka Tanzania kwenye ramani ya dunia kibiashara.

Aliwataka wawekezaji wengine kujitokeza kuwekeza kwenye sekta nyingine ikiwamo, madini, uvuvi, kilimo, ufugaji, dawa na uchumi wa buluu, akisisitiza kuwa Tanzania ni nchi nzuri kwa uwekezaji.

Mkurugenzi Mkuu anayeshughulikia masuala ya uchumi nchini Uswisi, Helene Artieda, alisema chemba hiyo itakuwa lango la biashara kati ya nchi hizo mbili, ili kuchochea uwekezaji na uhusiano wa kiuchumi.

"Kuundwa kwa chemba hii ni ishara nzuri ya ukuaji wa biashara, litakuwa jukwaa ambalo wafanyabiashara watabadilishana mawazo na kupanua fursa za kibiashara na uwekezaji, ili kujenga na kudumisha uhusiano imara," alisifu Helene.

Mkurugenzi Mkuu kampuni inayohusika na wawekezaji Tanzania (SHIKANA GROUP), Amne Kagasheiki, alisema lengo kubwa la chemba hiyo ni kuwaleta pamoja wafanyabiashara kutoka Uswisi na Tanzania kufanya biashara pamoja.

"Mimi ni mwekezaji kwetu hii ni fursa kubwa sana ukizingatia mimi ni Mtanzania niliyesoma na kuishi Uswisi kwa muda mrefu chemba hii itawasaidia wafanyabiashara wadogo kupeleka bidhaa zao Uswisi na kutengeneza bidhaa bora zitakazoweza kushindana kidunia," alisema Amne ambaye ni miongoni mwa waanzilishi wa chemba hiyo.

Shughuli hiyo ilifanyika nyumbani kwa Balozi wa Uswisi nchini, Didier Chassot, ikiwakutanisha pamoja wafanyabiashara, wawakilishi wa sekta binafsi na wanadiplomasia 120.



# CCM yapinga adhabu ya viboko 70 kwa vijana kabila la Wameru

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Arusha kupitia Jumuiya ya Wazazi kimepinga adhabu ya kuchapwa fimbo 70 kwa vijana wa Wilaya ya Arumeru wanaodaiwa kwenda kinyume na maadili ya kabila la Wameru.

Kimesema pamoja na hatua ya wazee wa ukoo (Washiri) wilayani humo kutumia mila zao kuwarekebisha vijana kwa kuwachapa fimbo ipo haja kutazamwa upya umuhimu wa kuendelea na mila hizo kwani zinachochea vitendo vya ukatili.

Katibu wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Arusha, Deogratias Nakey, aliyasema hayo jana mkoani hapa wakati akizungumza na wanachama wa CCM.

Alisema matukio ya ukatili yamekuwa yakishamiri kila wakati kutokana na maadili kuporomoka miongoni mwa jamii, hivyo aliwataka wananchi kukemea kwa nguvu zote na kuwa mstari wa mbele kufichua.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Wilaya ya Meru, Nangera Nanyaro, alisema suala la kuchapa viboko 70 kwa vijana wasio na nidhamu ni utaratibu walioukuta kutoka kwa wazee wa mila ila wataendelea kukemea adhabu hiyo.

"Kuchapa ni ukatili ila ni utaratibu uliowekwa na wazee wetu wa mila na desturi kwa lengo la kufundisha lakini naonya vijana walioharibika kitabia kwa unywaji wa pombe misibani na kwenye ibada,"alisema.

Aliongeza kuwa wataendelea kutoa elimu ili kuzuia matukio ya utovu wa nidhamu yasitokee ili viboko 70 visitumike.

Katibu wa jumuiya hiyo Wilaya ya Meru, Jane Mollel, alisema kuwa lengo la ziara hiyo ni kukagua uhai wa chama na kutoa elimu juu ya matukio ya ukatili katika kata mbalimbali wilayani humo.

Mshiri Mkuu wa Wameru, Ezroni Sumari, alisema suala la uchapaji fimbo 70 kwa vijana ni mila iliyowakuza na imekuwa msaada mkubwa kwa jamii hiyo na wamefanikiwa kudhibiti tabia mbalimbali ikiwamo ulevi na matusi kwa vijana.

Alisema viongozi wa siasa wanaopinga mila hiyo ya viboko ni namna ya kuomba kura kwa vijana na wao kama wazee wa mila hawataacha kutumia utaratibu huo.

"Fimbo 70 zipo na sisi kiutamaduni tumekuzwa na fimbo kutoka kwa wazazi wetu ndiyo maana tumeziweka katika maadili mtu huwezi kuchapwa zote 70, utachapwa tano na kukopeshwa 65 na endapo utajirekebisha zinafutwa,"alisema.

Alisema adhabu ya fimbo 70 imesaidia kurekebisha tabia za vijana ambao wengi wao walikuwa hawafanyi kazi wanashinda wakinywa pombe na hivi sasa wamebadilika na wanakwenda hata kanisani.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (kushoto), akizungumza na Mhandisi wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Wilaya ya Arusha, Albert Kyando (katikati), wakati alipokwenda kuangalia changamoto za miundombinu wezeshi kuelekea mradi wa Safari City, uliopo Burka Mateves jijini Arusha jana. **PICHA: WANMM**

## DC aeleza namna serikali ilivyoupiga mwingi wilayani kwake

**Na Dege Masoli,** KILINDI

MKUU wa Wilaya ya Kilindi Mkoa wa Tanga, Abel Busalama, amesema serikali imefanikiwa kufanya mambo makubwa wilayani humo ambayo hayakuwezekana kupatikana kwa vipindi vilivyopita.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati wa hafla ya utoaji mkopo wa bajaji na bodaboda uliotolewa na Halmashauri ya Wilaya hiyo.

Alisema kero kubwa ya barabara iliyokuwa inaikabili Wilaya ya Kilindi ikiwamo kutokupitika nyakati za mvua serikali imesikia suala hilo na kujenga.

Alisema serikali imeanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Wilaya ya Handeni kwenda Wilaya ya Kilindi kupitia Kwediboma hadi Singida jambo ambalo ni la kujivunia.

"Historia ya wilaya yetu ni barabara zake hazikuwa zinapitika kwa misimu yote ila serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan ameamua kuifuta kabisa kero, hivyo tujivunie mradi huu,"alisema Mkuu huyo wa Wilaya.

Hata hivyo, aliwataka wanufaika wa mkopo huo kuzitumia bajaji na pikipiki hizo kwa uangalifu ili ziweze kuleta tija sambamba na urejeshaji kwa kuwa itasaidia kutoa fursa kwa wengine kupata mkopo huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kilindi, Gracian Makota, alisema mkopo huo wa bajaji nne na pikipiki

38 umegharimu Sh.milioni 200.9 zinazotokana na asilimia kumi ya mapato ya ndani na yalitolewa kwenye vikundi vya vijana na watu wenye ulemavu.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Kilindi, Ndayahundwa Bilama, alisema mkopo huo umezingatia tatizo la usafiri uliyoko katika eneo hilo kwa kuwa kuna uhaba wa daladala.

Aidha, alisema bajaji hizo zitakuwa mbadala wa daladala kwa kuwa baadhi ya wananchi wamekuwa waoga wa kupanda pikipiki, hivyo watazitumia kwa safari zako.

# Wadau tanzanite wenye leseni zilizokufa wapewa siku 30

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

WAFANYABIASHARA na wachimbaji wa madini ya tanzanite eneo la Mirerani mkoani Manyara ambao leseni zao zimekwisha muda wa matumizi wamepewa muda wa mwezi mmoja kuzitolea maelezo vinginevyo watafutiwa.

Ofisa Madini Mkazi wa Mirerani, Menard Msengi, alitoa taarifa hiyo jana kwenye kikao kilichowajumuisha wachimbaji, wafanyabiashara wa madini ya tanzanite na mameneja wa migodi.

Msengi alisema leseni zote zinazodaiwa ada ya mwaka zinapaswa zilipiwe mara moja kabla wamiliki wake hawajapewa hati za makosa.


"Kumekuwa na maombi mengi kwenye mfumo ambao haujalipiwa, hivyo naelekeza maombi yote yawe yamelipiwa ndani ya siku 30 baada ya hapo maombi hayo yatafutwa," alisema Msengi."Kila mmiliki wa leseni anatakiwa kutekeleza masharti aliyopewa wakati anakabidhiwa leseni hiyo, ikiwa ni pamoja na kuandaa tathmini ya awali ya utunzaji mazingira (EPP) na awasilishe kiapo cha uadilifu,"alisema.

Hata hivyo alisema wachimbaji wote wawe wanaingia mikataba yenye tija na wafadhili, ili kuepusha migogoro ya mara kwa mara na mikataba hiyo lazima isajiliwe na ofisi ya Ofisa Madini Mkazi.

"Naelekeza mtu yeyote asiyekuwa na leseni ya broker asijihusishe kabisa na biashara ya kununua madini, madini yote yaletwe soko la madini hapa Mirerani," alisema.

Kadhalika wadau hao wa madini walifundishwa mada mbalimbali ikiwamo utaratibu wa matumizi na utunzaji sahihi wa baruti, usalama na afya katika maeneo ya uchimbaji na utunzaji na uhifadhi mazingira katika maeneo ya uchimbaji.

Pia walifundishwa ulipaji wa tozo mbalimbali za serikali na utunzaji wa kumbukumbu, udhibiti wa madini katika migodi na utaratibu wa utoaji wa taarifa za uzalishaji.





# Waliopisha ujenzi bomba la mafuta wakabidhiwa nyumba

**Na Restuta Damian,** MULEBA

BAADHI ya wananchi wa Kata ya Kalambi na Kasharunga wilayani Muleba mkoani Kagera waliopitiwa na mradi wa bomba la mafuta wamepewa nyumba kama fidia.

Wakazi hao ni wale waliopitiwa na mradi wa bomba la mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani mkoani Tanga.

Wakizungumza na Nipashe jana katika makabidhiano ya nyumba hizo, baadhi ya wananchi walishukuru serikali kwa kuwajali na kuwalipa fidia.

Mkazi wa Kijiji cha Kiguzi Kata Kalambi, Mary Alphonce, alisema awali waligoma kuhama wakidhani watafukuzwa katika maeneo yao bila kulipwa fidia.

"Niliwaza mimi na watoto wangu sita nitaenda wapi sehemu ya kuishi, tayari nyumba ya vyumba viwili na shamba la kulima vimechukuliwa, wapi nitapata eneo lingine, kumbe wenyewe walikuwa wanawaza kutujengea nyumba za moja wa moja ambazo zimekuwa zetu kabisa," alisema.

Mwananchi wa Kijiji cha Kiteme, Kata ya Kasharunga, Rahim Hussen, alisema hakuwa na uwezo wa kupata nyumba kwa hali ilivyokuwa katika familia yake na mazingira magumu aliyonayo, lakini fidia hiyo imekuwa mkombozi wao.

Alisema kuna faida ambazo amezipata katika mradi huo na kwamba licha ya kupata nyumba lakini alilipwa fedha ambazo zitamsaidia kuanzisha biashara.

Diwani wa Kata ya Kasharunga, Theobard Michael, alisema, wananchi wake walikuwa wanamuuliza kila wakati kwamba watahamia maeneo gani ya kuishi na familia zao endapo watapisha eneo hilo.

Alisema hali hiyo ilikuwa inampa wakati mgumu katika kuelimisha wananchi hao kwani hawakuwa na imani ya kupata makazi ya kudumu na za gharama kubwa.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC), Dk. Wellington Hudson, alisema wananchi hao wataendelea kupewa huduma ya chakula kwa kipindi cha mwaka mzima wakiwa kwenye makazi mpya.

Dk. Hudson alisema wananchi hao wamejengewa nyumba 15 kati ya 292 zitakazojengwa maeneo mbalimbali yaliyochukuliwa ili kupisha mradi huo.

Mkurgenzi wa mradi wa ujenzi wa bomba hilo, Martin Tiffen, alisema wananchi hao walipewa nafasi ya kuchagua wapewe fedha ama wajengewe nyumba.

Alisema wananchi zaidi ya 300 katika maeneo mbalimbali yaliyopitiwa na mradi walichagua kujengewa nyumba na kupewa kiasi kidogo cha fedha ili ziwasaidie kufanya shughuli za ujasiriamali.

# Kagera yapitisha matumizi ya bil.365/- mwaka 2023/24

**Na Titus Mwombeki,** KAGERA

KIKAO cha Kamati ya Ushauri mkoani Kagera kimewasilisha mapendekezo ya bajeti ya matumizi ya Sh. bilioni 365.3 kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Akiwasilisha taarifa hiyo kwenye kikao hicho, Katibu Tawala Msaidizi, Nesphory Bwana, alisema kuwa bajeti hiyo imeongezeka ukilinganisha na bajeti ya mwaka huu wa fedha.

"Mwaka wa fedha 2022/2023 tulikuwa na bajeti ya Sh. bilioni 354.4 na kwa mwaka huu mapendekezo yetu ni Sh. bilioni 365.3 na vyanzo vikuu ni mapato ya ndani ya halmashauri zetu, wadau pamoja na serikali, " alisema.

Alisema katika mapendekezo ya bajeti hiyo wamebainisha miradi 36 mikubwa na kuwa wataalamu wataendelea kuichambua ili kupata inayotakiwa kupewa kipaumbele ambayo itawasilishwa serikali kuu.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Albart Chalamila, aliwataka watumishi wa umma mkoani humo kuendelea kisimamia miradi mikubwa ya kimkakati ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na serikali.

"Serikali ili ifikie malengo yake ya kuwaletea maendeleo wananchi inategemea sana usimamizi wetu sisi watumishi tuliopewa dhamana, lazima tuhakikishe tunasimamia vyema fedha za miradi kwa maslahi mapana ya wananchi na taifa kwa ujumla," alisema.

Aidha, Chalamila alizitaka halmashauri kuhakikisha zinatafuta njia bora ya kutatua matatizo yanayowakabili wawekezaji na siyo kuwakatisha tamaa kwa kuwa mchango wao ni mkubwa katika mkoa huo.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Emmanuel Johnson (kushoto), akikabidhi fedha 64,000/- kwa mwanafunzi Kabula Sita anayesoma kidato cha kwanza katika Shule Sekondari Isoso wilayani humo jana kwa ajili ya kununua sare za shule pamoja na mwenzake, Kundi Singu, baada ya kuripoti kidato cha kwanza wakiwa na sare za shule ya msingi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wakulima wa pamba waomba wataalamu kuongeza uzalishaji

**Na Vitus Audax,** MWANZA

BAADHI ya wakulima wa pamba wilayani Sengerema mkoani Mwanza wameiomba serikali kuimarisha kilimo hicho hususani katika maeneo ya vijijini kwa kuweka wataalamu na kubuni mbinu mbadala katika uzalishaji.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti katika ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, walisema kwa sasa uzalishaji wao umejikita katika mbinu za kienyeji hatua inayosababisha uzalishaji kuwa chini tofauti na matarajio.

Mmoja wa wakulima hao, Alphonce Maneno: "Hapa nimelima kwa kutumia utaratibu wa kienyeji, sijatumia utaalamu wowote wala kuweka mbolea, hii imetokana na kutofikiwa na wataalamu nikaamua nilime tu nilivyozoea."

Akizungumza na wakulima baada ya kutembelea wakulima hao, Malima alisema bado uzalishaji upo chini kutokana na wakulima kulima kizamani.

"Kwa hali hii tunahitaji kuwa na kilimo cha kisasa katika zao hili na maamuzi yangu ni kuwasilisha mpango wa kuweka kilimo cha kisasa, Bodi ya Pamba nchini (TCB), baada ya kupata hekari za kutosha itawatumia wakulima ambao watakuwa tayari kuingia katika mpango huu," alisema Malima.

Mpango huo utawatumia wataalamu watakaopima udongo ili kutoa ushauri aina ya mbolea inayofaa kutumiwa na namna ya upandaji zao hilo kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo ili mkulima apate kilo 2,000 kwa hekari moja.

Aidha, Malima akiwa njiani kwenda mgodi wa Nyanzaga kupata taarifa za maendeleo ya fidia za wakazi jirani na eneo hilo, alisimama katika Kata ya Igarula na kuzungumza na wananchi.

"Niwasihi sana wananchi muwe na utulivu na msikubali kudanganywa na wachache watakaokuja kwa nia ya kuchochea migogoro wakati mkiwa mbioni kulipwa fidia na mgodi wa Nyanzaga," alisisitiza.

Aliwahakikishia wananchi kunufaika na mradi wa maji wa Sh. bilioni 13.7 unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (SEUWASA) wilayani Sengerema mkoani Mwanza.

Kuhusu uhaba wa mabweni katika Shule ya Sekondari Ngoma, Malima aliahidi kuwajengea mabweni mawili.


Ukurasa 12

NI KAMA SIMULIZI YA KUSADIKIKA ...
Mjasiriamali mwenye ulemavu kapambana hadi kusimama, leo ana ofisi na ameajiri



Ukurasa 13

Serikali imtazame Osam Milanzi kwa jicho la tatu

BUFE
IJUMAA MACHI 3, 2023
Nipashe


Ukurasa 14

**Moto wawaka Baraza la Madiwani Magu, kashfa kupotea mabati kwenye kituo afya**

DEREVA BAJAJI MZEE JULIUS MILAMBO...

# Mtumishi umma aliyesota mahabusu miaka kibao, kutoka anafikia kustaafu

**Na Neema Hussein, Mpanda**

MAISHA mara zote yanatajwa ni 'safari ndefu; unajua unakotoka si uendako. Mzee Julius Milambo (61) katika safari yake, alikuwa mtumishi wa umma, akakwama gerezani, anapokomboka mahabusu, akakuta ajira imetamati, sasa ni mstaafu anayeendesha bajaji.

Mzee huyo ni mkazi wa Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi, ambaye katika mazungumzo yake na Nipashe, anasimulia alikuwa mtumishi wa Halmashauri ya mkoa wa Katavi.

Anakumbuka alianza katika utumishi wakati wa mfumo wa chama kimoja kushika hatamu,akiwa Katibu wa Chama cha Mapinduzi wa Tawi la Mtakuja Inyonga, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlele. Hiyo ilikuwa kati ya mwaka 1985 na 1986.



Mzee Julius Milambo, akiwa katika biashara yake ya kuendesha bajaji. **PICHA: NEEMA HUSSEIN.**

Baadaye anasema, alihamishiwa katika kijiji cha Usevya, kilichoko katika Halmashauri ya Mpimbwe mwaka 1987 akiwa Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho.

Anasema mwaka 2001, tena akahamishwa kupelekwa kata ya Kabungu, katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika na ilipofika mwaka 2002, akateuliwa kuwa Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo.

Anasimulia safari ikamkuta tena mwaka 2003, akihamishwa katika kata ya Ugala na ilipofika mwaka 2006, akahamishwa tena kupelekwa katika Kata ya Utende, iliyopo kwenye wilaya ya Mlele na baada ya hapo tena, alihamishwa na kupelekwa katika kata za Mbede na baadaye Majimoto ndiko akakwama na janga la maisha.

**MKASA ULIVYOMPATA**

Mzee Milambo anasimulia kisa ambacho hatokisahau katika maisha yake, kilichomhamishia mahabusu ya Magereza kwa miaka sita, akitamka: "Kukaa mahabusu miaka sita kulitokea tatizo kwenye eneo la kazi ambako kipindi hicho nilikuwa (Ofisa )Mtendaji wa Kijiji cha Bujombe, Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika.

"Kulitokea mauaji kuna mtu alichomwa kisu, sasa katika 'kutajana tajana' wakawa wametaja mgambo waliokuwa wakizunguka kwenye eneo lile kufanya kama oparesheni, lakini tukio hilo lilitokea usiku wa saa saba, wananchi kama unavyojua hawawapendi mgambo.

"Kwa hiyo, wakasema ni mgambo fulani tulimfanganisha, sasa ikabidi mimi niambiwe '(Ofisa) Mtendaji tunamuhitaji huyo aliyetajwa'! Basi, nikamtafuta nikamkamata, nikawakabidhi polisi, basi wakaanza kuchukua hatua.

"Basi baada ya upelelezi ikaonekana sio kweli yule mgambo hakuhusika, basi akaachiwa. Mimi niliingia kama kiongozi kwa sababu yule mgambo kipindi anaulizwa hakufafanua.

"Aliulizwa hili tatizo kwanini limetokea na wewe umehusika, hii kazi mlikuwa mnafanya mlitumwa na nani? Akasema tulitumwa na Mtendaji, pasipo kutoa ufafanuzi kuwa ni kazi gani.

"Hao mgambo walikuwa wakifanya kazi ya kufuatilia Operesheni ya Usafi, yaani kuhamasisha wananchi kwamba jamani tunatakiwa kujenga makaro, tunatakiwa kuwa na vyoo, yaani usafi tu kwa ujumla.

"Basi nilivyotajwa mimi kwenda kule, nimekaa maana kipindi cha nyuma upelelezi ulikuwa unachukua muda sana. Kwa hiyo ilipelekea mimi nikakaa muda wote (gerezani), ila baadaye ikaonekana mimi sina hatia, nikawa nimeachiwa.

"Kukaa kule mahabusu, kumenisaidia kuwa inatakiwa niishi vipi na jamii na usikae tu ukabweteka, lazima utafute kazi ya kufanya," anasimulia.

Mzee Milambo anasema, baada ya kutoka mahabusu familia yake aliikuta iko chini sana kimaisha, wakati huo mke wake alikuwa akichoma vitumbua na kuuza mchele sokoni.

Anasema watoto aliowaacha wakiwa wanasoma shule ya awali, aliwakuta darasa la sita na mwingine aliyekuwa shule ya msingi alikuwa sekondari.

Milambo anasema wakati anakamatwa ilikuwa Desemba mwaka 2015 mwishoni na 2016 ndipo alianza kukaa mahabusu mpaka alipoachiwa mnamo Oktoba,2021.

Anakumbuka ilikuwa tukio la furaha kwa familia yake baada ya kuachiwa, huku watoto wake wakimwambia aliyoyakuta kama wameenda tofauti awasamehe.

Mzee Milambo sasa anaziomba mamlaka za dola za serikali, pale zinapomkamata mtu, zijaribu kufanya upelelezi wa kina mapema ili kupunguza siku za mtu huyo kukaa mahabusu na kuchelewa kuendelea na shughuli za ujenzi wa Taifa.

"Mimi kwa serikali kuhusu upelelezi naomba wajitahidi tu kuhakikisha na kuangalia haki ya mtu. Mimi najua haipotei, hata ufanyeje utaichelewesha tu lakini itafika siku yule mtu

**INAENDELEA UK.14**

BIASHARA

NI KAMA SIMULIZI YA KUSADIKIKA ...

# Mjasiriamali mwenye ulemavu kapambana hadi kusimama, leo ana ofisi na ameajiri

**Na Mary Mosha MOSHI**



Malisario Lyimo, akiwa na mwanawe Ofisa Masoko, Pendo Lyimo katika duka la bidhaa zake za ngozi, eneo la Mtei, Manispaa ya Moshi. **PICHA: MARY MOSHA.**

“NILIANZA kwa kushona malapa chini ya mti, nilikutana na matatizo mengi yakiwemo ya ubaguzi, kudharauliwa na watu mbali mbali wengine kukurusha mara baada ya kuwashonea malapa yao kwa kuwa huna cha kuwafanya,” anasema Malisario Lyimo.

Huyo ni mjasiriamali mwenye ulemavu wa viungo na baba wa watoto wanne kutoka eneo la Majengo kwa Mtei, mjini hapa, akiwa na umri wa miaka 60.

Anasema miongoni mwa ubaguzi aliokumbana nao ni pamoja kunyimwa hata nyumba za kupanga kwa kuhofiwa kushindwa kulipa fedha ya pango, kutokana na hali yake ya ulemavu.

“Niliumia sana bila kukata tamaa na badala yake, niliongeza jitihada za kufanya kazi na kujifunza zaidi ili nipate kuisaidia familia yangu, iliyokuwa ikinitegemea kwa hali na mali,”anaieleza Nipashe.

Lyimo anaeleza kwamba, licha ya matatizo mengi aliyopitia kila mara, hakukata tamaa na aliendelea kufanya kazi kwa bidii, huku akimuomba Mola.

Anasimulia kwamba amekuwa akikabiliwa na matatizo mengi kikazi na hasa ya ubaguzi, kunyanyaswa na hata wakati mwingine watu kumchonganisha na familia yake, waweze kuachana kwa miaka 20, sasa anajisifu kuvuka vikwazo kwa mafanikio, akiwa na ofisi yake.

Lyimo ni mjasiriamali wa bidhaa za ngozi, baba wa watoto wanne na mke, anayefanya biashara yake eneo la majengo kwa Mtei, akiwa na makazi alikojenga, Msaranga katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro.

“Mwanangu wa kwanza yupo chuo cha Ardhi jijini Dar es Salaam ameingia mwaka 2022 na namsomesha hivyo hivyo. Naamini Mungu hataniacha, hajapata mkopo kabisa na wa mwisho amemaliza VETA, nipo naye katika eneo langu la kazi akiwa kama ofisa masoko,”anasema.

**ALIVYOJIFUNZA UFUNDI**

Lyimo anasema alijifunza fani hiyo, baada ya kuona maisha yamekuwa magumu na hana namna ya kuilisha familia yake, pamoja na kutimiza majukumu yake kama baba na wakati huo huo mume. Anaeleza, licha ya hali yake, bado akatambua wajibu wake.

“ Kiujumla mwanzoni sikujifunza sehemu yoyote ujuzi wa kushona tofauti na kuwaona mafundi viatu wakifanya hivyo, ingawa baadhi ya mafundi walikuwa wakinidharau na kuona siwezi chochote.

“Ilinilazimu kutumia nguvu kubwa kujifunza, ikiwa ni pamoja na kupita kwenye maeneo wanayofanya kazi mafundi na kuwatazama wanachokifanya bila ya wao kujua na ninaporejea najikuta katika kufanya majaribio hadi naweza,” anasimulia Lyimo.

Anasema kutokana na hali ya kutokubalika, kuna wakati alikuwa akifukuzwa kwa mafundi hao mara anapokuja mtu mwingine au mteja, akidaiwa kupisha eneo hilo au aondoke, ili wateja wasikose pa kukaa kwa amani kutokana na uwapo wake.

“Ninapokwenda kupiga stori pamoja na kuiba ujuzi, hukaa nikipiga stori mbili tatu, ingawa anapokuja mtu mwingine (mteja au rafiki wa fundi) mimi hulazimishwa nikae chini, au kutakiwa

kuondoka au kuhamishwa kwenye kiti nilichokaa,” anatamka, akiongeza”

“Ili kupisha binadamu au kutupiwa majina ya kejeli’ huyu mlemavu amekuja kuniongezea tu nuksi nisifanye kazi’, aondoke watu tukae na kadhalika.”

Anasema alivumilia akiendelea kuwaza malengo yake ni kuhakikisha anayafikia kwa kujifunza kila mara na kufanya majaribio.

**SAFARI YA KUANZA ‘KUTOKA’**

Lyimo anasema, baadaye alimudu kushona (kurekebisha) viatu vya watu na baadhi wakaanza kumuamini kutokana na ufanisi wake, hasa akiwatoza bei ndogo wateja wake.

“Ujuzi wangu ulikuwa na nikaanza kutengeneza viatu vya watoto wadogo vya ngozi, kwa ‘kuigilizia’ vile vinavyokuja kuripea na kuwashauri baadhi ya wazazi kubadilisha soli za viatu vilivyotoboka. Baada ya kupata jina, nilianza kutafuta ngozi kwenye Kiwanda cha ngozi Moshi kisha kutengeneza viatu vya ngozi.

“Sio kazi rahisi, ila kwa jitihada iliwezekana, nilikuwa mdadisi wa mara kwa mara hata kule kiwandani, walinipa maelekezo na wengine walinikatia ngozi kwa mashine na nikaanza kujitafutia riziki kwa kiwango hicho,” anasimulia.

Kwa mujibu wa Lyimo, hapo ndipo akaanza kushuhudia maisha na yaliendelea, hata akaweza kuwafundisha vijana wanne kazi, pamoja na kuwaajiri katika utafutaji wa masoko.

Kutokana na tabia yake ya kupenda kujifunza kila mara, anasimulia akakutana na asasi ya kimataifa ya kiraia ya ‘Solidaridad Network’ kwenye mradi wake wa kuongeza thamani ya mazao ya ngozi, Zimbabwe na Tanzania.

Hapo Lyimo ana simulizi nyingine kwamba, waliweza kuwapatia mafunzo ya kina kuhusu utengenezaji bidhaa za ngozi na hasa viatu, pochi na mikanda.

**KINACHOMTATIZA SOKONI**

Lyimo analalamika kwamba, kwa sasa soko limekuwa tatizo kubwa, kwani umma kwa sehemu kubwa ni wateja wa bidhaa za kigeni akiziita ni ‘bandia’ na watu hao hawana uzalendo.

“Bado kuna tatizo la ngozi bora, kwani katika mkoa wa Kilimanjaro kuna viwanda vitatu tu vya uchakataji ngozi, lakini kwa sasa, moja kati ya hivyo kimefungwa na kusababisha wengi kuhemea ngozi kwenye hivyo viwili, ambavyo wakati mwingine hupata ngozi zisizo bora,” anaeleza.

“Ombi langu binafsi ni wafadhili na watu wenye mapenzi mema, kunisaidia ili niweze kupata mashine za kisasa zitakazonisaidia kufanya kazi zangu kwa urahisi tu.

“Kwenye upande wa masoko, tunaomba serikali kuangalia uwezekano wa upandishwaji kodi za kuingizwa bidhaa bandia (zisizo ngozi halisi) na kuhamasisha Watanzania kuvaa zaidi bidhaa za ngozi,” anasema .

Agustino Kimario (27), ni miongoni mwa vijana waliopata mafunzo na kufungua ofisi yake, anasema mara baada ya kujifungua mtoto wake alikabiliana na matatizo yaliyomlazimu mara baada ya mtoto kuhitimu miezi miwili alianza zoezi la kutafuta kazi bila mafanikio ndipo alipoanza kushona malapa nje kidogo ya nyumba yake.

“Pitapita zangu za hapa na pale, nilimuona baba mmoja mwenye ulemavu (mshona viatu), niliongea naye, nikamuomba anifundishe, ili kujiingizia kipato kwa kile nilichokiamini kuwa kama yeye ni mlemavu anaweza, mimi siwezi kushindwa.

“Nilipoongea naye, alinifundisha, nilielewa na kupitia vikoba, niliweza kukopa na kufungua ofisi yangu kwa sasa najitegemea,” anasimulia

Pia anaeleza kuwa, biashara yao hutegemea msimu na mwisho wa mwaka hadi mwanzoni mwa mwaka watoto wanapoenda shule.

“Kwa sasa nimeweza kujitegemea kiuchumi, kuwasomesha wadogo zangu na kumlea mama yangu, ambaye mara nyingi hutembea kwenye masoko kuuza. Kwa siku unaweza kuuza shilingi 70,000 hadi laki moja, ikiwa biashara ‘imechanganya’, ingawa kuna wakati hali inakuwa mbaya zaidi.

Rai yake ni kwamba, serikali ijitahidi kuwawekea wajasiriamali fursa ya masoko ya uhakika, mitaji na kuongeza jitihada kuhamasisha Watanzania kuacha kutumia bidhaa za plastiki wazame katika ngozi.

“Nimewahi kusikia juu ya asilimia 10 (mikopo) ya halmashauri, lakini imekuwa na milolongo mirefu sana, kiasi kwamba unakata tamaa.

“Unaweza kurudishwa zaidi ya mara tano, sita kwa ajili ya kitu kimoja.”anasema

**WADAU WALIOMVUSHA**

Julius Fanuel, Ofisa Miradi kutoka asasi ya kimataifa ya kiraia ya Solidaridad Network, anasema mradi wao umeweza kukutana na wajasiriamali wa ngozi mbalimbali nchini Tanzania na Zimbabwe.

Anafafanua kwamba nchini kwa sasa wamejikita katika miradi ya maziwa, kahawa, chai, dhahabu na ngozi, hivyo anataja walikijikita kuwa “asasi hii inayolenga kujenga dunia ambayo vyote vinavyozalishwa na kutumiwa vinatosheleza mahitaji ya sasa na baadaye pasipo kuathiri mazingira hasa katika kuongeza mnyororo wa thamani.

“Kwa Tanzania, inashughulika na kusaidia kutatua matatizo ya uzalishaji masoko kwa mnyororo wa thamani wa bidhaa kama vile kahawa, chai, maziwa na ngozi, hasa kwa wajasiriamani wadogo.

“Solidaridad inatekeleza mradi wa kuendeleza sekta ya ngozi uitwao ‘Promoting a Competitive , Inclusive and sustainable leather sector in Tanzania and Zimbabwe’...”anasema Ofisa Mradi.

Anafafanua kuwa, ni mradi unaofadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya, kupitia Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), ukitekelezwa mkoani Kilimanjaro, kwenye wilaya za Moshi, pia Manispaa ya Moshi .

Ni mradi uliozinduliwa na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Tixon Nzunda mwaka jana, akihimiza halmshauri hizo kuwapa kipaumbele wenye ulemavu, nao waweze kujinyanyua kiuchumi



Mandhari ya Manispaa ya Moshi, ambayo ndiyo soko lake kuu, fundi Malisario Lyimo.

## TAFAKURI YA MLALAHOI




## Serikali imtazame Osam Milanzi kwa jicho la tatu



NA JOSEPH KULANGWA
+255 713 410008
(kulangwasos@gmail.com)

TUKO msibani mtaani, mazishi yanaendelea, lakini kinachotawala hapa, ni mijadala mbalimbali kuhusu misiba na masaibu yanayowapata wafiwa baada ya kuondokewa na wapendwa wao.

Lakini linalosikika zaidi ni pale mtu anapolazwa na kufia hospitalini na kuibuka suala la gharama za matibabu na hifadhi ya mwili mochwari na jinsi uongozi wa hospitali unavyochachamaa kudai.

Watu wanaonesha kusikitishwa na hatua ya baadhi ya hospitali kuzuia miili mpaka hapo wafiwa wanapokuwa wamelipa gharama, ndipo waruhusiwe kuchukua mwili kwa maziko.

Wapo wanaofikia mahali kusema ni uonevu tu, kutokana na kwamba kabla ya mtu kufariki dunia amekuwa akilipa kodi kwa njia mbalimbali, ambayo ndiyo inawalipa madaktari na wauguzi mishahara yao lakini pia kununulia dawa.

Wanasema hivyo, baada ya kuona kwamba mtu akishapoteza maisha hubadilishwa na kuwa kama bidhaa ambayo wanauziwa ndugu ambao wanalazimika kulipia gharama za dawa, malazi, chakula na hifadhi ya chumba cha maiti.

Wanashangaa na kupendekeza kwa Serikali kuondoa dhana hiyo ya kudai gharama pale mtu anapokuwa amepoteza maisha, kwani anakuwa hana kazi tena kwa ndugu zake, ambao si tu wamempoteza, lakini wanatakiwa tena kuny’ang’anywa hata walichobaki nacho.

Mmoja wa wanaojadili hilo anafikia kutolea mfano wa gari bovu lililoharibika likapelekwa kwa fundi gereji, lakini likashindikana, anahoji mantiki iko wapi kwa mmiliki wa gari hilo kulazimishwa kulipia matengenezo wakati halikutengemaa.

Anasema ni sawa na binadamu, anaugua, analazwa hospitalini juhudi za madaktari zinagonga mwamba na anapoteza maisha, inakuwaje sasa ndugu kudaiwa kulipa gharama za kitu kilichopotea ambacho hata hivyo hakitawasaidia tena maishani!

Mwingine anakuja na hoja, kwamba ni bora Serikali ikajitazama upya na kulinganisha kati ya elimu na matibabu kipi kilipiwe na kipi kitolewe bure. Anahitimisha kwa kutaka bora wananchi walipie elimu na kupewa matibabu bure.

Hoja yake, ni kwamba siku hizi elimu haina maana kama zamani, kwa sababu zaidi ya kujua kusoma na kuandika na kukaririshwa, baada ya hapo mtoto akishahitimu hata chuo kikuu, atarejea nyumbani kusumbua wazazi wake baada ya kukosa ajira.

Anasema ni tofauti na matibabu ambapo mtu akiyakosa ndio unakuwa mwisho wa maisha yake, huku asiyekwenda shule akiweza kuishi kwa kujitafutia chochote cha kufanya na kujiingizia kipato. Mantiki iko wapi hapo? Unayesoma hapa tafakari nawe pia. Nikiendelea kusikia mijadala hii inayofikirisha, kichwani inanijia taswira ya ile video iliyosambaa hivi karibuni kwenye mitandao ya kijamii, ikimwonesha mkazi wa Manzese, Dar es Salaam, Osam Milanzi, akizolewa na basi la mwendokasi karibu na makutano ya barabara za Jamhuri na Morogoro.

Kwa aliyeiona video ile, bila shaka akili ilimtuma kuwa pale alipokuwa amebamizwa Milanzi, lazima alibaki vipande vipande kwa kusagwa na basi lile ikizingatiwa ukubwa wa gari lakini pia mwendo lililokuwa nao na pale alipobananishwa.

Nilikuwa mmoja wa walioamini hivyo, lakini pia sikuamini niliposikia Milanzi yuko hai Muhimbili amelazwa chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalumu (ICU) akiweza kutamka jina lake moja tu; Osam.

Nilithibitisha yuko hai, baada ya kumwona mkewe, Isha Mohammed na mdogo wake, Shaban Milanzi wakiwa Muhimbili kumjulia mpendwa wao na kusema anaendelea vizuri na anajitambua na kuzungumza! Sikuamini, nikasema kumbe Mungu mkubwa!

Lakini nikawapongeza wafanyakazi wa Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) kwa walichokifanya kupigania maisha yake na sasa huenda Mungu akamsaidia akarudi kwenye kibarua chake cha kujitafutia kula na familia yake.

Kilichoniuma na kunigusa zaidi, ni pale Isha alipofunguka na kusema mumewe ni masikini na hana bima ya afya na hivyo kutarajia gharama kubwa ya matibabu yake, na akaomba Serikali imsaidie kwa hilo, ili mumewe akipona wasiandamwe na madeni ya matibabu.

Alisema hivyo akizingatia kibarua alichonacho mumewe, ambacho ni cha kipato cha kijungujiko tu, ambacho kwa makadirio ya haraka haraka, hakitamwezesha kulipia gharama za matibabu hayo ya mumewe.

Naamini Serikali sikivu ilimsikia Isha ambaye alionesha uchungu dhahiri hasa baada ya kumtafuta mumewe kwa siku sita bila mafanikio na kujikuta ameangukia MOI. Watu aina ya Isha na familia yake ni wengi nchini, ni vema ukawapo utaratibu mbadala hata kama si wa bima ya afya kwa wote.

UCHUMI

# Moto wawaka Baraza la Madiwani Magu, kashfa kupotea mabati kwenye kituo afya

- Zakutwa majumbani zimeshaezekwa...
- Fedha 'asilimia 10 mikopo' zasitishwa



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu, Simon Mpandalume, akiongoza kikao cha Baraza la Madiwani. **PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS.**

**Na Anthony Gervas, Mwanza.**

ULIKUWA moto kwenye kikao cha Baraza la Madiwani Magu, pale tuhuma za kupotea mali za mradi huo ikigubika mjadala na kugusa madai ya wizi wa vifaa vilivyokuwa vya ujenzi wa kituo cha afya kata ya Shishani wilayani humo.

Ni hoja zinazoelekeza kidole moja kwa moja, kwa mtendaji mwandamizi wa kata Shishani na mlinzi katika kituo kimoja cha afya na mganga.

Ikaelezwa kikaoni, vifaa vilivyobainiwa na kukamatwa katika uchunguzi wa jopo la madiwani, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Mpandalume Simon ni mabati 81 yaliyonunuliwa na serikali kila moja shilingi 55,000 yalikutwa yameezekewa nyumba mbalimbali za watu binafsi katika kata hiyo.

Mwenyekiti Simon akakiambia kikao hicho kwamba, baada ya kuyakamata mabati hayo kwenye nyumba hizo, wamiliki wa nyumba hizo binafsi walihojiwa na kukiri kuuziwa na watumishi hao.

"Baada ya kuyakamata mabati hayo yakiwa yameezekewa nyumba za watu binafsi katani hapo, wenye nyumba walikiri kuuziwa na watumishi hawa akiwemo mlinzi wa kituo hicho kwa bei ya shilingi 35,000 kila bati moja ambalo serikali imenunua shilingi 55,000 kila moja," anasema Mwenyekiti Simon.

Vifaa vingine vilivyokamatwa ni vigae maboksi matano vilivyokuwa vimefichwa shambani kwa kuchimbiwa chini, pia vifaa vya ujenzi ' jipusam'.

Mwenyekiti Simon anabainisha kuwa, katika kudadisi wizi huo, mlinzi wa kituo cha afya akakiri kushirikiana na watumishi hao kuzitoa kwa awamu, baada ya kuahidiwa kupewa fedha, lakini baadaye walimpa fedha kidogo tofauti na makubaliano yao, hivyo na yeye akaamua kuiba mabati matano akayauza.

Pia,akafafanulia kikao akimnukuu mlinzi kwamba aliamua kutoboa siri nzima ya wizi alipobanwa, huku watuhumiwa wengine wamekataa kukiri kuhusika, wakimuelekezea dai mlinzi.

Baraza la Madiwani wilayani humo likalalamika, pia kushangazwa na kitendo kilichofanywa na watumishi wa serikali, wakamuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Fedelica Myovella, awachukulie hatua za kisheria watuhumiwa, ikiwamo kuwasimamisha kazi kupisha uchunguzi.

Ni suala lililoungwa mkono na madiwani wote waliomtaka Mkurugenzi Mtendaji kutekeleza maagizo yao ya kuwasimamisha kazi watumishi wanaotuhumiwa kujihusisha na wizi.

Makamu Mwenyekiti pia wa halmashauri hiyo, Faustine Makingi, anaungana na ombi la kuwachukulia hatua, ikianzia na kuwasimamisha kazi wahusika wanaotuhumiwa na kashfa hiyo.

"Tunakuagiza baraza hili, Mkurugenzi kuwachukulia hatua watumishi hawa waliohusika na wizi wa vifaa vya ujenzi wa kituo hicho cha afya kata ya Shishani, ikiwamo kuwasimamisha kazi kupisha uchunguzi zaidi uendelee," anatamka Mwenyekiti Simon.

Katika kikao hicho cha bajeti ya robo ya pili ya mwaka wa fedha 2023/24, Mwenyekiti akaeleza kushangazwa na wahusika wanaokabiliwa na tuhuma za wizi, kuendelea kuonekana kazini pasipo Mkurugenzi Mtendaji kuchukua hatua stahiki za kiutumishi.

Vilevile, Mwenyekiti Simon akaeleza kukerwa na kitendo cha kuwasilishwa taarifa za miradi ya maendeleo ya kata hiyo, pasipo kuingizwa taarifa za wizi wa vifaa hivyo, akidai "kuna siri nyuma ya pazia ikiendelea."

**BAJETI ILIYOZU JAMBO**

Katika halmashauri hiyo bajeti ya mwaka wa fedha 2023/24, imepitisha kiasi cha shilingi bilioni 4.8, baada ya kuona uwezo wake umeongezeka, huku Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali ya Mitaa (TAMISEMI) ikiwaongezea shilingi milioni 100, hata bajeti hiyo kufikia shilingi bilioni 4.9 kutekeleza miradi ya maendeleo wilayani humo.

Kuhusu fungu la fedha zinazotolewa na halmashauri kwa vijana,wanawake na wenye ulemavu kupitia vikundi, Mwenyekiti Simon anaeleza kuwa zipo shilingi milioni 300 katika akaunti ya halmashauri hiyo.

Anasema fedha hizo zimesitishwa kutolewa kutokana na udanganyifu wa watendaji na viongozi wa serikali, kwamba wanasajili vikundi baadhi vikiwa 'hewa' na majina yake hayaeleweki.

Simon anazitaka kamati za maendeleo ya kata, kusaidia kusimamia vikundi hivyo ili kujiridhisha na uhalali wa vikundi hivyo, kabla ya kupatiwa walichoomba.

Mwenyekiti anasisitiza haja ya kutolewa elimu katika mikutano ya hadhara, ikiwamo ya kisiasa.

Anasema watendaji wa serikali wana wajibu wa kuhakikisha wanaielimisha jamii kufahamu yote yanayofanywa na serikali, kuanzia ngazi ya juu na namna inavyowanufaisha, wilayani Magu.

**KAULI YA MKURUGENZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu, Fedelica Myovella, anakiri kuwapo tukio la wizi na anapokea agizo la Mwenyekiti wa Halmashauri na Baraza la Madiwani kuwasimamisha kazi watumishi wanaoshukiwa, ili wapishe uchunguzi.

"Watendaji na watumishi wa serikali wasimamie vema miradi ya maendeleo, fedha zilizopelekwa katika miradi ya maendeleo kutoka mapato ya ndani ni asilimia 65, maelekezo ya serikali ni asilimia 40 kupeleka serikalini," anasisitiza Myovella.

Myovella anawataka watendaji wa vijiji na kata kutoa taarifa za mapato na matuimizi ya miradi ya maendeleo ya wananchi inayotekelezwa, kila baada ya miezi mitatu, ili kuondoa udanganyifu unaojitokeza.

## MTUMISHI UMMA ALIYESOTA MAHABUSU MIAKA KIBAO, KUTOKA ANAFIKIA KUSTAAFU

**INATOKA UK.11**

mtakua naye pamoja na uvumilivu ndio unaotakiwa, maana bila uvumilivu sijui ingekuaje.

"Na ucheleweshwaji wa hizi kesi zinasababishwa na wananchi wenyewe kutokujitoa kwa haraka kutoa ushahidi mda mwingine mashahidi wanapotafutwa kwamba wewe utakuwa shahidi wanakimbia au wanakwepa, sasa wanaipa serikali tena mzigo wa kuendelea kusubiri mpaka inafika mahali wanalaumiwa," anasimulia.

**MAISHA MAPYA**

Hapo anasimulia kwamba, baada ya kutoka mahabusu alirejea kazini kupata haki zake. Kwa sasa amejiajiri kuendesha bajaji yake, inayomuingizia kipato. "Nilipokuwa huko (gerezani) muda wangu ulifika wa kustaafu miaka 60. Nikajiona bado nina nguvu, nafanyaje shambani? Mashamba sikuweza kujiwekeza, ikabidi niamue kutafuta kazi ambayo naweza kujiajiri, ikawa kununua bajaji hii hapa (anaionyesha).

"Nimenunua toka mwaka jana. Kwa kweli inanisaidia sana kuniingizia kipato cha kupata 'mia mbili mia mbili' ambazo zinanisaidia kuishi na familia yangu na watoto wanasoma na wajukuu," anaeleza.

Mzee Milambo anasema kupitia biashara yake ya bajaji, kwa siku anaweza kuingiza kipato cha shilingi 35,000 hadi shilingi 50,000 na endapo atatoka nyumbani asubuhi na kuwahi abiria wanaoenda stendi wanaosafiri saa 12 kwa mabasi yaendayo mikoani, humuongezea kipato,ikilinganishwa na mshahara aliokua akipata kipindi cha utumishi.





## Washindi kampuni bunifu chipukizi kujulikana leo

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu ya mkononi ya Vodacom inatarajia kutangaza kampuni bunifu chipukizi tatu zilizoibuka washindi wa msimu wa pili wa programu ya 'Vodacom digital accelerator' iliyofanyika kwa kushirikiana na Smart Lab.

Washindi hao watapatikana baada ya kuwasilisha na kuonyesha shughuli wanazozifanya kwa jopo la majaji waliobobea kwenye maeneo ya teknolojia, ujasiriamali, uwekezaji na sheria.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi wa Huduma za Kidigitali, Vodacom, Nguvu Kamando, alisema uwasishaji wa maonyesho hayo unatarajiwa kufanyika leo.

Alisema msimu wa pili wa programu hiyo ulianza Aprili mwaka jana na kuruhusu maombi kutoka kwa kampuni zote za kibunifu chipukizi za kiteknolojia za kitanzania zenye mustakabali wa kukua.

Alisema katika maombi hayo kampuni 12 zilichaguliwa kujiunga na programu hiyo na kuingia kwenye hatua ya kujengewa uwezo ambapo zilipatiwa msaada wa ziada kwenye kukuza mikakati yao ya kimasoko, eneo la kiufundi na kuwaunganisha kwa washirika na wawekezaji.

Alisema kampuni hizo bunifu zinatoka kwenye sekta tofauti ambazo ni pamoja na huduma za kiteknolojia za kifedha, afya, biashara za mtandaoni, elimu, kilimo na usalama wa mtandaoni.

Komando alisema: "Ningependa kutoa wito kwa wadau kwenye sekta ya ubunifu na teknolojia kujisajili kwa njia ya mtandaoni ili kushiriki wakiwa popote walipo siku ya kesho".

Alizitaja kampuni bunifu chipukizi ambazo zimefikia hatua ya fainali kuwa ni pamoja na Shule Yetu Innovations, Smart Darasa, Lango Academy na Vijana Tech, kwa upande wa huduma za elimu za kiteknolojia, Hack it Consultancy inawakilisha eneo la huduma za usalama wa mtandaoni.

Nyingine ni Seto, Twenzao, Get Value na Spidi Africa ambazo zipo chini ya biashara za mtandaoni.

Alizitaja zingine ni Medpack ikiwakilisha huduma za afya za kiteknolojia, Bizy Tech Pamoja na Bizzy Pay ambazo zipo upande wa huduma za kifedha za kiteknolojia.

# JKT yaandaa mfumo wa kuwafuatilia wanaohitimu mafunzo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Kujenga Taifa (JKT) linaandaa mfumo wa kuwafuatilia vijana wanaohitimu mafunzo ya kujitolea ya jeshi hilo ili kufahamu maendeleo yao wanapokuwa katika jamii zao.

Aidha, limesema halitanunua mchele na mahindi katika maduka, kwa sababu wanachakula cha kujitosheleza kutokana na uzalishaji wanaofanya katika kambi mbalimbali za jeshi zilizopo hapa nchini.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Rajabu Mabele, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya miaka 60 ya Jeshi hilo toka lianzishwe.

Meja Jenerali Mabele alisema, vijana wengi wanaopita katika mafunzo hayo wanafanya vizuri katika shughuli zao za ujenzi wa taifa ambazo wanakwenda kujiajiri wao wenyewe.

"Tunapata mrejesho vijana wengi wanaohitimu mafunzo ya kujitolea wanafanya vizuri katika fani mbalimbali, tunaandaa mfumo kuwafuatilia ili kujua maendeleo yao,"alisema Meja Jenerali Mabele.

Akizungumzia kuhusu suala la chakula, Meja Jenerali Mabele alisema jeshi hilo limeweka mkakati kuhakikisha ifikapo mwaka 2025 liwe linajitegemea kwa chakula ili kupunguzia mzigo wa kibajeti serikali.

Alisema JKT pamoja na majukumu yake ya ulinzi, kupitia Shirika la Suma JKT, linajishughulisha na shughuli mbalimbali za uzalishaji mali na huduma kwenye sekta za ujenzi, uhandisi, sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi, viwanda pamoja na huduma na biashara, lengo ikiwa ni kuzidi kujiongezea kipato.

Alisema moja ya mafanikio ambayo wameyapata hadi sasa ni pamoja na kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo na maeneo mengine ambayo yameboreshwa. Akizungumzia kuhusu maadhimisho ya miaka 60 ya JKT iliopangwa kufanyika Julai 10, mwaka huu katika Uwanja wa Jamhuri Dodoma, Meja Jenerali Mabele alisema mgeni rasmi anatarajia kuwa Rais Dk. Samia Hassan Suluhu.

Alisema katika maadhimisho hayo, JKT hilo limepanga kufanya shughuli mbalimbali za kijamii, ikiwamo kuchangia damu, kufanya usafi wa mazingira katika maeneo mbalimbali, ikiwamo hospitali, kutoa msaada wa kibinadamu kwa watoto yatima na upandaji miti ili kuifanya Dodoma kuwa ya kijani.

Naye Mkuu wa Tawi la Utawala JKT, Brigedia Hassan Mabena, alisema maadhimisho hayo yataongozwa na kaulimbiu isemayo 'Malezi ya vijana, uzalishaji mali na ulinzi kwa ustawi wa taifa'.

Mbali na hilo alisema, JKT pamoja na majukumu yake ya msingi ya malezi ya vijana uzalishaji mali na ulinzi, limekuwa ikifanya maboresho mbalimbali kuendana na wakati pamoja na mabadiliko ya sayasi na teknolojia.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maadhimisho hayo, Kanali George Kazaula, alisema maandalizi yanaendelea vizuri, huku akizikaribisha taasisi mbalimbali kushiriki.




Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali Rajabu Mabele, akizungumza na waandishi wa habari, Chamwino mkoani Dodoma juzi, kuhusu maadhimisho ya miaka 60 ya jeshi hilo, yanayotarajiwa kufanyika Julai 10 mwaka huu. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# TPHPA yawanoa wakulima, maofisa ugani kuhusu afya

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAMLAKA ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) imetoa mafunzo kwa wakulima, maofisa ugani na wauzaji wa viuatilifu wapatao 215 ili kulinda afya ya walaji, wanyama na mazingira.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TPHPA, Prof. Joseph Ndunguru, alibainisa hayo juzi jijini hapo alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za mamlaka hiyo kwa waandishi wa habari.

Alisema katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya mamlaka hiyo katika mwaka 2022/2023 wametekeleza shughuli mbalimbali ikiwamo mafunzo kwa wakulima, wauzaji wa viuatilifu na maofisa ugani ambao watasaidia kulinda afya za walaji, wanyama na mazingira.

Aidha, alisema mamlaka imeendelea kuwajengea uwezo wakaguzi wa mimea na mazao waliopo katika mipaka ya nchi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa njia ya mafunzo.

Alisema wakaguzi 72 wa afya ya mimea wamepatiwa mafunzo kutoka vituo vya Rusumo, Kabanga, Mutukula, Mrusagamba, Kibirizi, Mabamba, Manyovu, Bukoba port, Mwanza Port, Sirari.

Wengine kutoka Holili, Tarakea, Namanga, Tanga port, Horohoro, Dar es Salaam port, Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Julius Nyerere, Mtwara port, Uwanja wa Ndege wa Songwe, Tunduma, Kasumulo na Mtambaswala.


Kadhalika, alisema mamlaka kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo imefanya uchambuzi wa sampuli za udongo takribani 1,300 kutoka kwenye mashamba ya "Block farming" na matokeo ya uchambuzi yatawezesha kutoa ushauri. "Mamlaka pia imepima afya za watumiaji wa viuatilifu 403 kwenye mashamba ya maua ambapo watumiaji 70 sawa na asilimia 17.36 walipatikana na viwango vidogo vya masalia ya viuatilifu, hivyo ushauri ulitolewa kwa wahusika,"alisema Dk. Ndunguru.

Alisema jukumu lingine ambalo limefanywa na mamlaka ni ukaguzi ili kudhibiti visumbufu vya kikarantini ambapo jumla ya mashamba na kampuni 16 yalikaguliwa na jumla ya sampuli 102 zilichunguzwa.

Vile vile alisema mamlaka imekusanya sampuli 400 za nasaba za mimea ya aina mbalimbali na kuhifadhi katika benki ya mbegu.

Akizungumzi kuhusu udhibiti wa viwavi jeshi vamizi alisema wakulima 2,987 na maofisa ugani 16 katika kata 16 za Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero walipatiwa mafunzo.

Pia mbinu za kudhibiti nzi wa matunda zilitolewa kwa wakulima 849 na maofisa ugani saba katika Wilaya ya Handeni kipindi cha Julai 2022 hadi Februari 2023.





## Madiwani waagiza viazi vitamu kuanza kulipiwa kodi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA.

MADIWANI wa Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wametaka viazi vitamu kuingizwa kwenye mfumo wa ulipaji wa kodi kama yalivyo mazao mengine ya biashara, ili kuongeza mapato ya ndani.

Wamesema zao hilo likianza kulipiwa ushuru litaongeza mapato ya halmashauri na hivyo kufikia lengo la makusanyo ya Sh. bilioni 32.6 kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mazao mengine yanayotakiwa kuingizwa katika mfumo huo ni mtama, ulezi pamoja na uwele ambayo kwa sasa hayatozwi ushuru wa mazao katika masoko, minada na magulio.

Diwani wa Kata ya Sabasabini, Emmanuel Makashi aliyabainisha hayo jana katika kikao cha kawaida cha baraza la madiwani cha robo ya pili ya mwaka wa fedha 2022/2023.

Alisema bila kuibua vyanzo vipya vya mapato na kuvisimamia vile vya zamani itakuwa ngumu kufikia lengo la makusanyo waliojiwekea katika mwaka huu.

Alisema ili kuongeza mapato ya ndani ya halmashauri ni vyema mazao ya viazi vitamu, mtama, ulezi na uwele vikaingizwa kwenye mfumo wa utozaji wa ushuru wa mazao.

Diwani mwingine, MichaelBundala alisema baadhi ya mashine za ukusanyaji wa mapato katika masoko, minada na magulio mbalimbali hazifanyi kazi na taarifa za ubovu wake zimesharipotiwa katika ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Gagi Lala aliagiza viazi na mazao mengine ambayo hayapo kwenye mfumo wa mapato yaingizwe na ukusanyaji ufanyike mara moja.

Pia alimwagiza Mkurugenzi kuhakikisha mashine mbovu zinazotumika katika ukusanyaji wa mapato zinatengamaa ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani alisema, halmashauri hiyo inategemea mapato yake ya ndani kwa kiwango kikubwa kupitia kilimo na wamewahamasisha wananchi kulima kwa wingi mazao ya chakula na biashara.

Alisema msimu huu pamba imelimwa kwa wingi ikilinganisha na vipindi vilivyopita na amehakikisha maofisa ugani wa kata 20 wanapata vyombo vya usafiri.

Aliongeza kuwa pikipiki 37 zimeshafika kwa ajili yao, lengo likiwa ni kuendelea kuhamasisha kilimo kwa tija ili halmashauri inapata mapato yake.

Wakati huo huo, wakulima tumbaku katika Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga wameliangukia baraza la madiwani kuliomba kuzibana kampuni zilizonunua zao hilo kuwalipa fedha.

# Serikali kuongeza idadi ya miradi inayogusa wananchi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

SERIKALI imeahidi kuongeza miradi ya wananchi ikiwamo ya elimu ili kuwanufaisha katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Ahadi hiyo ilitolewa juzi mkoani Mwanza na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Jenista Mhagama wakati akizungumza na wananchi wa vijiji vya Ihayabuyagu na Igekemaja.

Alisema Wilaya ya Magu itaendelea kunufaika na miradi mbalimbali ya kuwaletea maendeleo wananchi kwa kuongezewa mingine 10 katika mwaka huu wa fedha.

Aliongeza kuwa hatua hiyo italenga sekta ya elimu kwenye ujenzi wa madarasa manne na maabara moja katika Shule ya Sekondari Igekemaja ambayo bado haijaanza kutumika rasmi.

Akizungumza na wananchi katika vijiji hivyo baada ya kuvitembelea na kukagua miradi inayosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), alisema serikali kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuharakisha maendeleo ya wananchi na kwamba viongozi katika maeneo husika wanatakiwa kuisimamia.

Alisema ushirikiano wa wananchi katika kuchangia asilimia 10 ya ujenzi wa miradi inayotekelezwa na TASAF ni muhimu na kwamba umefanikisha kukamilisha nyumba ya wahudumu wa afya pamoja na vyumba vya madarasa katika shule mpya ya sekondari inayotarajiwa kuanza kutumika hivi karibuni.

Mhagama alisema kutokana na uhitaji wa shule hiyo aliahidi kutatua mahitaji ya muhimu yaliyopo kwa kushirikiana na wizara zenye dhamana ikiwamo kuweka nishati ya umeme shuleni hapo pamoja na huduma ya maji.

Alisema serikali kupitia awamu ya tatu ya mradi wa TASAF itajenga maabara ya kisasa shuleni hapo pamoja na madarasa mengine manne ili kukidhi mahitaji ya wananchi wa kata hiyo.

Alisema licha ya serikali kutoa fedha za utekelezaji wa miradi ya TASAF kwa wakati katika maeneo mbalimbali nchini bado anashangazwa kushindwa kutekelezwa kwa muda uliopangwa, hivyo kuitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuichunguza ili kubaini kama kuna ubadhirifu.

Katibu Tawala Msaidizi Mipango na Uratibu wa Mkoa wa Mwanza, Joachim Otaru alisema anatambua miradi hiyo ya TASAF kwa kuwa inaleta mageuzi chanya kwa wananchi wa mkoani humo.

Aliahidi kushirikiana TAKUKURU katika kuifuatilia ili kuhakikisha inaendelea kuwa na tija kwa wanufaika.

Mkuu wa Wilaya ya Magu, Rachel Kassanda alisema TASAF wametoa Sh. milioni 103 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya na Sh.milion 64 kujenga vyumba vya madarasa mawili ya Sekondari ya Igekemaja.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, akizungumza na wananchi wa mtaa wa Igekemaja kati, kata ya Kisesa, mkoani Mwanza juzi, baada ya kukagua ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na ofisi ya mwalimu katika shule mpya ya sekondari inayotarajiwa kuanza kutumika hivi karibuni na kumaliza mrundikano wa wanafunzi kwenye sekondari ya Kitumba yenye wanafunzi zaidi ya 2700. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Wahimizwa kupata chanjo ya ugonjwa wa corona

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI wamehimizwa kuendelea kujitokeza kupata chanjo ya ugonjwa wa corona ili kupata kinga dhidi ya ugonjwa huo endapo watapata maambukizi.

Mratibu wa Elimu ya Afya kwa Umma mkoani Shinyanga, Mwita Thomas alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na vyombo vya habari na kuwaomba watumie kalamu zao kuhamasisha wananchi waendelee kujitokeza kupata chanjo hiyo.

Alisema ugonjwa wa corona bado upo na kwamba wananchi wanapaswa kuendelea kuchukua tahadhari ya kujikinga ili wasipate maambukizi, ikiwamo kunawa mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji tiririka, kupata vitakasa mikono.

"Waandishi wa habari tumieni kalamu zenu kuongeza uelewa kwa jamii dhidi ya kupata chanjo ya ugonjwa wa corona, chanjo hii ni salama haina madhara yoyote na watu wote ambao wamechanja hakuna aliyelalamika kupata tatizo lolote na imekuwa msaada mkubwa kwao kuwakinga," alisema Mwita. Aidha, alisema katika mkoa huo wamejiwekea malengo ya kupandisha kiwango cha kuchanja wananchi hadi asilimia 120, kwamba mpaka sasa wamefikisha asilimia 108 na kubainisha kuwa chanjo hiyo inatolewa bure kwenye maeneo yote ya huduma za afya.

Ofisa Ufuatiliaji kutoka Shirika la Afya, Plus Chimombo, alisema kwa mwaka huu wanatekeleza programu ya kuhamasisha wananchi kupata chanjo ya ugonjwa wa corona katika Manispaa ya Shinyanga na Wilaya ya Kishapu na kuahidi kutoa ushirikiano kwa waandishi wa habari kufanya kazi pamoja.



# ‘Wizara ya Afya ina jukumu la kutoa elimu lishe ya watoto

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya imesema kupitia kitengo cha lishe ina jukumu la kuelimisha jamii juu ya ulishaji bora wa watoto wachanga na wadogo.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Wizara ya Afya Zanzibar, Hassan Khamis Hafidh wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na mwakilishi la Pandani, Prof. Omar Fakihi Hamad.

Prof. Fakihi alitaka kufahamu mpango wa serikali kuhakikisha kwamba kila mtoto anapewa lishe bora kwa ajili ya ukuaji na kupata kinga bora ya mwili.

Akitoa ufafanuzi wa swali hilo, Waziri Hassan alisema elimu hiyo hutolewa kupitia vyombo vya habari na maofisa wa lishe kwa kushirikiana na wahudumu wa afya wa kujitolea ambao huwafuatilia watoto wenye lishe duni.

Alisema pia hufanya mikutano ya midahalo kwenye jamii ya kuhamasisha matumizi ya vyakula vinavyopatikana kwa urahisi kwenye jamii kwa ajili ya watoto wao.

Alisema uhamasishaji wa unyonyeshaji wa maziwa ya mama hufanyika kwa sababu maziwa ya mama ni kinga bora kwa mtoto lakini pia humkuza mtoto akiwa na lishe bora na kupunguza athari za utapiamlo.

Naibu Waziri huyo alisema Wizara ya Afya ina mpango madhubuti wa kuongeza wataalamu ili kupunguza vifo vya watoto wakati wa kuzaliwa.

Alisema wafanyakazi 638 wameajiriwa wa kada mbalimbali katika vituo vya afya na hospitali ili kupunguza vifo vya watoto wachanga.

Aidha, alisema nafasi 177 zimeshatangazwa wenye sifa waombe na kuajiriwa kama taratibu za ajira zinavyoelekeza.

Kadhalika Waziri Hassan akijibu swali la mwakilishi wa Viti Maalum, Fatma Ramadhan, aliyetaka kujua ulipwaji wa posho za mapumziko kwa madaktari, alisema kumekuwa na ucheleweshwaji wa malipo ya posho za muda wa ziada kwa madaktari, kutokana na upatikanaji mdogo wa fedha za ruzuku na fedha hizo hulipwa kwa awamu kadri hali ya fedha inaporuhusu

Alisema Hospitali ya Mnazi Mmoja inakabiliwa na uhaba wa madaktari bingwa watakaokidhi mahitaji ya huduma kwa wananchi wote.

Alisema hospitali hiyo hupanga zamu za madaktari waliopo kwa uwiano sawa bila ya kujali siku au muda wa kazi.

Alisema: “Kunakuwa na ratiba ya madaktari wa wito ambapo uhitaji unapotokea basi madaktari waliopo zamu za wito hulazimika kuja kazini kusaidia kutatua tatizo”.



Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Zanzibar, Shamata Shaame Khamis, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi Chukwani, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ yakiri kutoweka kwa miti ya asili ikiwamo mlangilangi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Zanzibar imekiri kutoweka kwa baadhi ya miti ya asili ikiwamo mlangilangi ambao ni mti wa asili na wenye faida kiuchumi na kijamii.

Waziri wa wizara hiyo, Shamata Sahaame Khamis, aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la mwakilishi wa Mwanakwerekwe, Ameri Abdallah, aliyetaka kujua kiwango cha kupotea kwa mti huo.

Waziri huyo alisema wizara yake ipo katika harakati za kurejesha upandaji wa mti huo, akisema una faida nyingi za kiafya, kiuchumi na kiutamaduni. Alisema kiafya ni tiba ya maradhi mbalimbali kwa magonjwa ya mwanadamu.

Alisema kwa upande wa kiuchumi mti huo unafaida zaidi kwa nchi za asili zikiwamo Thailand, India na Ufilipino ambapo hutoa ajira kwa watu ambao hufanya kazi katika mashamba makubwa yanayopandwa miti hiyo kwa ajili ya kupata malighafi ya kutengenezea manukato na vipodozi. “Kiutamaduni mlangilangi ni kama ilivyo kwa mti wa kilua na asumini. Hapa Zanzibar maua ya mlangilangi hutumika kwa urembo na mapambo ambapo huchanganywa na mafuta ya nazi kwa kutoa harufu nzuri yenye kuvutia ambayo hutumika kwa kujipaka na ususi wa nywele”alisema.

Aidha, alisema serikali imeanza kuandaa mkakati wa kuirejesha Zanzibar katika uhalisia wake wa kijani kupitia programu ya urejeshaji wa urithi wa kijani.

Alisema programu hiyo inalenga kuotesha na kupanda miti mbalimbali ya asili ukiwamo mlangilangi.

Alisem serikali ilianza kubaini upoteaji wa mti wa mlangilangi tangu mwanzoni mwa miaka ya 1990, hivyo, Sheria ya Usimamizi na Uhifadhi wa Misitu Namba 10 ya mwaka 1996 imeutaja mlangilangi kuwa ni miongoni mwa miti iliyo hatarini kutoweka na kuhifadhiwa kisheria.

Waziri huyo alisema mti wa mlangilangi ni miongoni mwa miti inayokuwa haraka ambayo katika mazingira rafiki hukua hadi kufikia urefu wa mita 40. Alisema mti huo maua yake ndiyo hutumika zaidi kuliko kigogo na majani na duniani zipo aina 20 za jamii ya milangilangi, lakini kwa Zanzibar kuna aina moja inayojuilikana kitaalam kwa jina la ‘Canaga odorata’ ndio inayoweza kuota na kumea vizuri.

## Unguja yaongoza kutembelewa watalii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Muhammed Said, amesema Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja ndiyo unaongoza kwa kuwa na vivutio vingi vya utalii Zanzibar.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la mwakilishi wa Mwanakwerekwe Amer Abdallah aliyetaka kujua ni maeneo gani Zanzibar yanayoongoza kwa kuwa na vivutio vingi vya utalii.

Waziri huyo alisema hali hiyo pia imesababisha kutembelewa zaidi na wageni wanaofika Zanzibar na inakadiriwa kwamba asilimia 80 ya wageni wanaotembelea Zanzibar hutembelea maeneo hayo.

“Maeneo hayo ni Mji Mkongwe, Visiwa vya Changuu, Chumbe, Bawe na Chapwani. vilevile kuna maeneo ya utalii wa kujivinjari ya Kisiwa cha Kwale (Safari Blue) na Fungu la Nakupenda. Mashamba ya viungo yaliyopo Kizimbani na Dole, Msitu wa Masingini, na maeneo ya kihistoria ya Maruhubi, Beit el Mtoni na Mahamamu ya Kidichi”alisema.

Waziri huyo alisema mkoa wa pili kwa kuwa na vivutio vingi ni Mkoa wa Kusini Unguja ambao unachukua nafasi ya pili baada ya Kaskazini Unguja kwa kutembelewa na wageni wingi.

Alisema vivutio vinavyopatikana ni Msitu wa Jozani ambao ni maarufu kwa uwepo wa kimapunju ambao huwezi kuwapata sehemu nyingine duniani.

Aidha, alisema mkoa huo pia kuna mradi wa vipepeo katika Kijiji cha Pete, mapango ya kihistoria ya kuumbi huko Jambiani, Miza wa Miza na msikiti wa kihistoria na Pomboo huko Kizimkazi.

Waziri Simai alisema sehemu hizo za Mkoa wa Kaskazini Unguja zinasifika kwa kuwa na fukwe nzuri.

Kwa Kisiwani Pemba alisema kuna Msitu wa Ngezi, Kisiwa cha Misali, eneo la kihistoriala Mkamandume na Kidike ni maeneo maarufu ambayo yanatembelewana wageni kwa wingi na Kidike ni eneo maarufu kwa uwepo wa popo wakubwa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


## PATA MKOPO KWA HARAKA

PATA MKOPO KWA HARAKA
**HADI 200,000,000/=**
KUTOKA
**ENTERPRISE FINANCE LIMITED**
KWAAJILI YA DHARURA MBALIMBALI KAMA KULIPA KODI YA NYUMBA, KUNUNUA GARI, KUBORESHA BIASHARA N.K

**TUNAPATIKANA**
DAR ES SALAAM **0677111333**
NA ARUSHA **0677226960.**


---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI**
**Kituo cha KINONDONI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Shauri la Madai Ndoa Na. 249/2022**
**Jina la mdai: DIAMOND TRUST BANK TANZANIA LTD**
**Jina la Mdaiwa: UPENDO GEOFREY KATIYUHAGILA**

### KUITWA SHAURINI MDAIWA

**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa: UPENDO GEOFREY KATIYUHAGILA WA MBAGALA, NZASA**
**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba**
**UNAAMRIWA KUFIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 16 Mwezi wa 03 Mwaka 2023 saa 8:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 22Mwezi wa 2 Mwaka 2023.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
KINONDONI
WILAYA YA KINONDONI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA- MWANZA**
**MAOMBI NA 165 YA 2022**
**MAUNGO LADSLAUS KAWA.........MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**YULITHA PIUS KULWA............MJIBU MAOMBI**

### WITO WA KUITWA MAHAKAMANI
### KWA: YULITHA PIUS KULWA

Unafahanmishwa kwamba Mleta maombi hapo juu amefungua shauri/Ombi dhidi yako katika Baraza la Ardhi na Nyumba Mkoa wa Mwanza, Ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 11/04/2023 katika Chumba cha baraza, jengo liko mkabala na Mahakama ya Mwanzo Mwanza Mjini Barabara ya Makongoro.
Kwa hivyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza siku hiyo wewe mwenyewe, wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria kujibu ombi hilo.
KAA- Ukijua kwamba ukishindwa kufika siku hiyo, Baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila nyie kuwepo.
Imetolewa nami kwa Amri na Chapa ya Baraza hii leo tarehe 01/03/2023.

MURIRYA N.
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) MWANZA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya**
**DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO**
**MKOA DODOMA**
**Usimamizi wa Mirathi Na 13/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU IDDI MPAMANDA MTALIKA WA CHANG'OMBE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA NA NASRA IDDI MTALIKA**

### TANGAZO

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/ maslahi yeyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 07/ Mwezi 03 Mwaka 2023 kabla huyo muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo
**Zingatia**
Endapo kama yeyote mwenye wosia wa Marehemu waweza kuleta mahakamani kukaguliwa. Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika
Imetolewa leo Tarehe 01 Mwezi 03 Mwaka 2023

HAKIMU

---


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HOSIANA WILHELM DIYAMET** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 340 DTN – TOYOTA RUSH.** Chassis No. **J200E0027304.** Engine No**. 3SZ2519970.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/79162/2023.**


---

## NYADHI INVESTMENT Co. LIMITED
## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**M/HAKIMU MKAZI MWANZA – SHAURI LA MADAI NA . 5/2022**
**JOHN KIMORI _____MDAI**
**DHIDI YA**
**ADAM BALENGA _____ MDAIWA**
**MM/MWANZA MJINI – SHAURI LA MADAI NA.07/2017**
**PRAXEDA MANASE _________MDAI**
**DHIDI YA**
**SAMORA HEBERT_____MDAIWA**
**M/MWANZO ILEMELA – SHAURI LA MADAI NA. 115/2019**
**TUMAINI JAMES NDONGO _______MDAI**
**DHIDI YA**
**JAMES NDONGO SANGA________MDAIWA**

KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA, MAHAKAMA YA MWANZO MWANZA MJINI NA MAHAKAMA YA MWANZO ILEMELA, TUNAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI AMBAZO NI NYUMBA NA KIWANJA. MNADA UTAFANYIKA MAHALA MALI ILIPO.

| SN | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | NYUMBA PLOT NA. 10 KITALU "P" | MTAA WA RUFIJI - MWANZA | 29/03/2023 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 2 | NYUMBA 1 | IPULI-MAHINA WILAYA YA NYAMAGANA MKOA WA MWANZA. | 30/03/2023 SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 3 | NYUMBA 3 | NYAMANORO WILAYA YA ILEMELA MKOA WA MWANZA | 30/03/2023 SAA 7 MCHANA NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA:**
1. KWA MALI INAYOHAMISHIKA, MSHINDI WA MNADA ATALIPA PESA YOTE ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA MARA BAADA YA KUTANGAZWA MSHINDI.
2. KWA MALI ISIYOHAMISHIKA, MSHINDI ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATALIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE. KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA.
3. MTEJA ANATAKIWA KUKAGUA MALI KABLA YA MNADA KUANZA.
4. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.

**MAWASILIANO: 0768-588155**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......17/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: BERNADETHA CHARLES NANDONDE WA NGERENGERE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**YALIYOLETWA NA CEDRIC CHARLES**

### TANGAZO

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 06 Mwezi 03 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 21 mwezi 02 mwaka 2023**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO M.

---

**IN THE DISTRICT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No 18 of 2023**
**In the matter of the estate of the late CARLOS LUKAS GACHA of Ntyuka within Dodoma Region**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by COLIN CARLOS GACHA**

### GENERAL CITATION

**(Rule 75 of Probate Rules Gn 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claining to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 24 day of 03 2023

Dated at Dodoma this 23 day of 02, 2023

RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ...........TANGA**
**Kituo cha MJINI TANGA...........Mkoa...TANGA**
**Usimamizi wa Mirathi Na................46/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: JOSEPHINE ANORD NGOWO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA: EPHATA DANIEL LEMA**

### TANGAZO

**(Kanuniya 5(2) yakanunizaUsimamiziwaMirathiMahakamazaMwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo tarehe 8 mwezi 3 mwaka 2023 kabla, huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
*Wosia wamarehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
*Marehemu hakuacha wosia
Imetolewa leoTarehe ....01... mwezi ...03...mwaka 2023

HAKIMU
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MJINI TANGA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......18/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: OMARY KIBWANA ALLY WA UKWELE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**YALIYOLETWA NA MIRAJI OMARY KIBWANA**

### TANGAZO

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 08 Mwezi 03 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 22 mwezi 02 mwaka 2023

**HAKIMU MFAWIDHI**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO
Hakimu

---

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT REGISTRY**
**AT MUSOMA.**
**MISC. LAND APPEAL No. 63 OF 2022**
**(Arising in Land Appeal No. 44/2021, in District Land and Housing Tribunal of Tarime, Original Land Case No. 69/2020 Ward Tribunal of Kemambo)**
**NYANGI MARWA ...............APPELLANT**
**VERSUS**
**KUBYO MBUSIRO.........RESPONDENT**

**TO: KUBYO MBUSIRO,**
**C/O V.E.O-NYABICHUNE VILLAGE,**
**TARIME.**

### SUMMONS FOR PUBLICATION

WHEREAS the Appellant have filed an appeal against you, you hereby summoned to appear in this court in person or by pleader duly instructed and able to answer all material questions relating to the appeal or who shall be accompanied by some person able to answer all such questions on the 7th day of MARCH, 2023 at 13:00 Pm o`clock in the forenoon before Hon. F.H.MTULYA, Judge to answer the case.
Take notice that, in default of your appearance on the day before mentioned, the Appeal will be heard and determined in your absence.
Given under my Hand and the Seal of the Court this 22nd day of March, 2023.

DEPUTY REGISTRAR
MUSOMA.
Deputy Registrar
High Court Of Tanzania
Musoma

---


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ANDREW CYPRIAN CHIMAZI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 128 CNL – TOYOTA NOAH.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB/81559/2023.**



## OFISI ZA MATANGAZO

***Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042,***

***Dar es Salaam. Mobile: +255 - 745 700 710.***

***E-mail: advertise@guardian.co.tz,***

***Website: www.ippmedia.com***

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Uganda yajitetea kuifunga ofisi ya Umoja wa Mataifa

**KAMPALA, Uganda**

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, ametetea uamuzi wa serikali yake kusitisha shughuli za Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa (OHCHR) nchini humo.

Utetezi huo ameutoa wakati akijibu swali la mwanahabari ambaye alihoji uamuzi wa Uganda kufunga shughuli za tume hiyo juzi, wakati wa kongamano la uwekezaji kati ya Uganda na Afrika Kusini mjini Pretoria.

"Hii ni kwa sababu tuna Tume ya Haki za Binadamu ya Uganda ambayo imeagizwa na katiba. Hivyo kuwa na nyingine ambazo si sehemu ya mfumo wetu wa katiba si jambo la lazima, lakini ni jambo la kutofautiana," alisema Museveni.

Aliongeza "Badala ya kwenda kuripoti kule ambako hatua zinaweza kuchukuliwa, wanaenda UN. UN inaweza kufanya nini Uganda? Hawana mamlaka ya kutekeleza."

Mnamo tarehe 3 Februari, Wizara ya Mambo ya Nje ya Uganda ilitangaza kuwa serikali haitakuwa na mkataba mpya na OCHCR, ambayo inamalizika muda wake mwishoni mwa Machi.

Katika barua hiyo iliyoenda ofisi kuu ya OHCHR, wizara ilisema kuwa Uganda imeendeleza uwezo wa kufuatilia, kukuza na kulinda haki za binadamu bila msaada kutoka nje.

Wanaharakati wamelaani uamuzi wa nchi hiyo kuifunga ofisi ya Umoja wa Mataifa, wakisema kuwa ni jambo la aibu.

Wakosoaji hao wanaona hatua hiyo kama taswira ya mwitikio wa serikali kwa uchunguzi unaoongezeka wa dhuluma, mateso, kutoweka kwa watu, utekaji nyara, kuwekwa kizuizini bila kesi na kukamatwa kwa watu walioachiliwa kisheria na mahakama. *BBC*



Mfanyakazi wa kikosi cha uokoaji akiendelea na kazi ya kuwaondoa abiria kwenye mabehewa baada ya treni mbili kugongana karibu na mji wa kati wa Ugiriki wa Larissa juzi. **PICHA: EPA-EFE**

# Abiria wajeruhiwa angani ndege ikipata misukosuko

**PORT LOUIS, Mauritius**

ABIRIA 17 wamejeruhiwa, wawili kati wakiwa katika hali mbaya baada ya ndege ya Shirika la Ndege la Condor kutoka Frankfurt, Ujerumani, kuelekea Mauritius kukumbwa na misukosuko ikiwa angani.

Ndege hiyo ilipata msukosuko uliotokana na hali mbaya ya hewa ilipokuwa ikiruka karibu na Madagascar saa mbili kabla ya kutua nchini Mauritius.

Picha za ndani ya ndege hiyo zilionesha kukiwa na uharibifu mkubwa.

Kulingana na taarifa ya polisi wa Mauritius, ndege hiyo aina ya De 2314 ilikuwa na abiria 270 wakati ikiruka.

Hata hivyo, iliweza kutua kwa dharura katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Mauritius mwendo wa saa 6:40 saa za ndani.

Timu ya dharura iliwahamisha abiria waliojeruhiwa hadi hospitali ya karibu.

"Kulingana na taarifa za awali, tukio hilo lilitokea karibu na Madagascar," Inspekta Shiva Coothen wa ofisi ya polisi ya Mauritius alisema.

"Mamlaka inasubiri ripoti ya kapteni ili kubainisha mazingira yanayozunguka tukio hili," aliongeza.

Mauritius wiki iliyopita ilikumbwa na Kimbunga Freddy ambacho kilisababisha safari za ndege zisitishwe.

Sehemu kubwa ya ukanda wa kusini mwa Afrika imekuwa ikikumbwa na mvua kubwa katika wiki za hivi karibuni. *BBC*

## Prince Harry, mkewe waamriwa kuondoka nyumba ya kifalme

**LONDON, Uingereza**

MWANAMFALME Harry na mke wake Meghan Markel, wameombwa kuondoka katika nyumba yao inayofahamika kama Frogmore Cottage iliyoko nchini Uingereza.

Msemaji wa wanandoa hao, amethibitisha suala hilo na kueleza iliripotiwa kwamba nyumba hiyo iliyoko katika uwanja wa Windsor Castle, ilikuwa imetolewa kwa Duke wa York.

Hata hivyo, kasri la kifalme la Buckingham Palace haijatoa kauli yoyote.

Harry na Meghan kwa sasa wanaishi California na watoto wao wawili, Archie na Lilibet.

Waliacha maisha kama washiriki wa familia ya kifalme mnamo 2020 na kuondoka nchini Uingereza muda mfupi baadaye.

Frogmore Cottage, nyumba ya daraja la II yenye vyumba 10 ndani ya uwanja wa Windsor Castle huko Berkshire, ilitolewa kama zawadi kwa wanandoa wa kifalme kutoka kwa marehemu Malkia.

Inasemekana waliambiwa waondoke kwenye nyumba hiyo na kasri la Buckingham mnamo Januari, siku chache baada ya Harry kuchapisha kitabu cha kumbukumbu yake ya maisha yake alichokiita 'Spare'. *BBC*

## Makombora yaua watatu Ukraine

**KYIV, Ukraine**

POLISI nchini Ukraine imesema kuwa watu watatu wameuawa na wengine wanne kujeruhiwa baada ya vikosi vya Russia kufyatua kombora katika jengo la ghorofa katika mji wa Zaporizhzhia.

Idara ya serikali ya Ukraine inayotoa huduma ya dharura ilibaini katika ripoti yake kuwa watu 11, waliokolewa kutoka kwenye kifusi cha jengo hilo lililoporomoka.

Hata hivyo, uvamizi wa Russia nchini Ukraine unatazamiwa kuwa mada kuu katika mkutano wa Mawaziri wa Mambo ya Nje wa kundi la G20, unaofanyika mjini New Delhi nchini India.

Wajumbe wa Ulaya na Marekani wamesisitiza kuwa wataiwajibisha Russia katika mzozo huo, huku Ujerumani ikisema kuwa ingetumia mkutano huo kukabiliana na propaganda za nchi hiyo.

Wakati huo huo, Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz, amesema Ujerumani na washirika wake walikuwa kwenye mazungumzo na Ukraine kuhusu mustakabali wa dhamana ya usalama katika maandalizi ya amani endelevu katika nchi hiyo.

Scholz aliyasema hayo katika hotuba yake mbele ya bunge la Ujerumani jana, na aliongeza kuwa nchi yake itaendelea kuiunga mkono Ukraine kwa kuipatia silaha. *DW*

# JKT KUADHIMISHA MIAKA 60 KWA MASHINDANO YA RIADHA

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

JESHI la Kujenga Taifa (JKT) limeandaa mashindano ya mbio za riadha (JKT Marathon 2023), ambayo yamepangwa kufanyika Juni 25, mwaka huu katika viwanja mbalimbali vilivyoko jijini hapo ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 60 ya jeshi hilo.

Mashindano hayo yanatarajia kushirikisha watu wa rika tofauti kutoka mikoa yote hapa nchini, wakiwamo wananchi na taasisi mbalimbali.

Akizungumza jijini hapo jana, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Jenerali Rajab Mabele, alisema mbio zitakuwa za kilomita tano, kilomita 10 na kilomita 21.

Mabele alisema kilele cha sherehe hizo kitafanyika Julai 10, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Jamhuri na mgeni rasmi atakuwa, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

"Tunaomba raia na taasisi mbalimbali zijitokeze kushiriki katika mashindano haya," alisema Mabele.

Aliongeza lengo la mashindano hayo ni kusherehekea miaka 60 ya JKT lakini ni moja ya mazoezi kwa ajili ya kujenga afya kwa jamii.

Kiongozi huyo alisema kila baada ya miaka 10 jeshi hilo huadhimisha sherehe hizo ambazo huenda sambamba na wiki ya JKT ambayo itaanza ifikapo Julai Mosi hadi 9, mwaka huu.

Sambamba na hilo siku ya kilele cha maadhimisho hayo, kutakuwa na bonanza la michezo mbalimbali ambayo itafanyika kwenye viwanja vya Nyerere Square na Chinangali Park.

Aliitaja michezo itakayoshindaniwa katika bonanza hilo ni soka, netiboli na wavu huku akisema pia kutakuwa na burudani mbalimbali kutoka kwa vikundi vya sanaa na maonyesho vya JKT.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya mashindano hayo, Kanali George Kazaula, alisema maandalizi ya sherehe hizo zinazodhaminiwa na Benki ya CRDB, NMB na Kampuni ya Simu ya Tigo yanaendelea vizuri.




Mashabiki wa Simba na Yanga wa mikoa ya Kanda ya Ziwa ambao ni washindi wa promosheni ya Betika Mtoko Kibingwa wamekabidhiwa mfano wa tiketi kwa ajili ya kuja Dar es Salaam kushuhudia mechi ya dabi itakayochezwa Aprili 16, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Betika Mtoko yafanya usaili

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI washindi wa Betika Mtoko wa Kibingwa kutoka mikoa mbalimbali nchini wakikabidhiwa tiketi zao za ndege kwa ajili ya kuja Dar es Salaam kushuhudia mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga, usaili kwa mashabiki walioshinda waanza kufanyika.

Mechi ya watani wa jadi itafanyika Aprili 16, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Washindi 20 kati ya 100 watakaoshuhudia mechi hiyo ya watani wa jadi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara tayari wamepatikana katika promosheni hiyo ya tano ya msimu wa kibingwa inayoendeshwa na Kampuni ya Michezo ya ubashiri ya Betika Tanzania.

Droo nyingine itaendelea leo kwa ajili ya kupata washindi wengine, Ofisa Habari wa Betika Tanzania, Juvelinaus Rugambwa, alisema na kuongeza kila wiki washindi 10 watakuwa wanapatikana.

"Ni rahisi kushinda, weka mikeka yako mitano ya kuanzia Sh. 500 na Betika, hata kama ikichanika bado una fursa ya kuingia kwenye promosheni ya Mtoko wa Kibingwa na kupata fursa ya kuishuhudia dabi kwa gharama za Betika," Rugambwa alisema.

Tayari washindi 20 wamepatikana katika droo hiyo itakayowapa tiketi mashabiki 100 kushuhudia dabi hiyo na watakaa katika eneo la VIP kwa gharama za Betika Tanzania.

## KMC FC yapania kuimaliza Mtibwa

**Na Adam Fungamwango**

KMC imejipanga kuichapa Mtibwa Sugar katika mechi ya hatua ya 16 bora ya mashindano ya Kombe la FA itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Manungu Complex ulioko Turiani, Morogoro.

Ofisa Habari wa KMC FC, Christina Mwagala, aliliambia gazeti hili jana wamejiandaa kikamilifu ingawa wanajua mechi hiyo itakuwa na upinzani.

Mwagala alisema timu yao ina historia safi wanapocheza na timu hiyo nyumbani na ugenini.

"Tunahitaji kufanya vizuri katika mchezo huo ili tuingie kwenye hatua ya robo fainali, vijana wamejiandaa vyema. Mchezo wa keshokutwa ni mgumu, lakini lazima tuwafunge Mtibwa, hatujawahi kupoteza mechi hata moja tukicheza nao hapa Dar es Salaam, tumekuwa tukiwafunga na tukienda kwao tunatoka sare,"alisema Mwagala.

Mechi nyingine za Kombe la FA zitakazochezwa kesho ni kati ya Ihefu dhidi ya Pan African, Singida Big Stars itawaalika JKT Tanzania huku Jumapili Azam watawavaa Mapinduzi FC na Kagera Sugar itapambana na Mbeya City.

## Wachezaji karate kupewa mafunzo

**Na Shufaa Lyimo**

WACHEZAJI wa mchezo wa karate kata pamoja na kumite wanatarajiwa kushiriki katika mafunzo maalumu yatakayofanyika kuanzia Machi 11 hadi 21, mwaka huu, jijini Dar es Salaam chini ya wakufunzi, Sensei Fulgence na Sensei Thadei, kutoka nchini Burundi.

Msemaji wa Chama cha Karate Tanzania, Salma Abdallah, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwaongezea ujuzi wachezaji wa hapa nchini ili waufahamu vyema mchezo huo.

"Mafunzo hayo yatawasaidia wachezaji kuufahamu vizuri mchezo huu pamoja na kujiandaa kufanya vyema kwenye mashindano yaliyopo mbele yetu," alisema Salma.

Aliongeza mchezo huo kwa sasa unazidi kupata umaarufu tofauti na miaka ya nyuma jambo ambalo linasaidia kuutangaza.

"Tunafurahi kuona sasa mchezo unapendwa, vipaji vipya vinazaliwa, tunaomba Watanzania wajiunge na mchezo wetu," aliongeza.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CITY YAMUWANIA RICE
KLABU ya Manchester City imejitokeza kuwania saini ya kiungo wa kati wa England, Declan Rice, mwenye umri wa miaka 25, ikiwa West Ham watashawishiwa kuachana na nahodha wao anayekadiriwa kuwa na thamani ya pauni milioni 100. ***(TeamTalk)***

### KEAN AMCHAMBIA RICE
KIUNGO wa kati wa zamani wa Manchester United, Roy Keane, amesema Declan Rice "hajapiga hatua" kule West Ham. ***(ITV, Metro)***

### SILVA BADO NJIA PANDA
MUSTAKABALI wa kiungo wa kati wa Ureno, Bernardo Silva katika klabu ya Manchester City "hauko wazi" huku Barcelona wakiendelea kufuatilia hali ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, kama yuko tayari kuhama iwapo ataruhusiwa kuondoka msimu wa joto. ***(Sport)***

### AOUAR AIKATAA UNITED
KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Houssem Aouar, mwenye umri wa miaka 24 amekataa kuhamia Manchester United na kukubali kujiunga na Eintracht Frankfurt ya Ujerumani mara mkataba wake katika klabu ya Lyon ya Ufaransa utakapokamilika msimu huu. ***(Daily Express)***

### NAPOLI YAIBANIA CHELSEA
NAPOLI inalenga kumpa mkataba mrefu mshambuliaji wa Georgia, Khvicha Kvaratskhelia, mwenye umri wa miaka 22 ambaye amekuwa akihusishwa na Chelsea na Newcastle United. ***(Gazzetta dello Sport)***

### STERLING KUBAKIA CHELSEA
WAKALA wa mshambuliaji wa England, Raheem Sterling, amesema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 hataki kuondoka Chelsea msimu wa joto - huku kukiwa na ripoti zinazomhusisha na Arsenal. ***(Sky Sports)***

### MOTING MALI YA STOKE
MSHAMBULIAJI wa zamani wa Stoke City, Eric Maxim Choupo-Moting (33), amekubali mkataba mpya wa mwaka mmoja na mabingwa wa Ligi Kuu Ujerumani, Bayern Munich. Mfaransa huyo alikuwa akihusishwa na kurejea katika Ligi Kuu England akihusishwa na na Manchester United au Tottenham Hotspur. ***(Sky Sports)***

### SCOTT AGOMBEWA ENGLAND
KLABU ya West Ham imejiunga na orodha ya timu zinazomfuatilia kiungo wa kati wa Bristol City, Alex Scott, mwenye umri wa miaka 19, ambaye thamani yake ni pauni milioni 25. ***(Daily Mail)***

### KARIUS ATAJWA MILAN
KLABU ya Inter Milan inavutiwa na mlinda mlango wa Newcastle United, Loris Karius, mwenye umri wa miaka 29. ***(FC Inter News, via Caught Offside)***

### ELNENY, ARSENAL SAFI
MCHEZAJI wa Timu ya Taifa ya Misri, Mohamed Elneny, amesaini mkataba mpya Arsenal utakaompeleka kuishi klabuni hapo hadi Juni 2024. Mkataba wake ulikua unamalizika Juni mwaka huu ***(Arsenal).***

### GERNACHO KUBAKIA UNITED
MCHEZAJI Alejandro Garnancho amekubali kusaini mkataba mpya wa muda mrefu na Manchester United ambayo kwa sasa imeonekana kuimarika zaidi ikiwa chini ya Kocha, Eric Ten Hag. ***(Skysport)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA: HATUACHI KUTAFUTA UBINGWA

**Kocha huyo atamba wataendelea kupambana katika kila mechi mpaka...**

**LONDON, England**

MIKEL Arteta amewapa changamoto wachezaji wake wa Arsenal na kuwataka kutochoka katika harakati zao za kuwania taji la Ligi Kuu England baada ya kupaa kileleni kwa pointi tano mbele ya Manchester City, akisema: "Hatutaacha."

Mabao mawili ya Gabriel Martinelli, pamoja na mabao kutoka kwa Bukayo Saka na Martin Odegaard, yalisaidia Arsenal kuwafunga Everton mabao 4-0 katika mchezo wa Jumatano.

Wakati Arsenal walianza pole pole dhidi ya vijana hao wa Kocha, Sean Dyche, baadaye waliongeza kasi na kushinda mechi yao ya tatu ya ligi mfululizo na kuambulia ushindi wao wa 100 wa Ligi Kuu England dhidi ya Everton.

Ushindi mkubwa wa Washikabunduki hao umewafanya wawapite City wanaoshika nafasi ya pili kwa pointi tano.

Alipoulizwa kama ushindi huo wa Arsenal dhidi ya Everton umewafanya kuwa na nafasi nzuri zaidi ya kutwaa kombe, Arteta alisema: "Unajua jibu langu hapo!

"Ninachopenda kila mtu ana shauku ya kufanya, na hatutazuia hilo - lazima tuendeleze.

"Lakini namna ya kukuza hilo ni kwa kuutazama mchezo huu na kuelewa tunatakiwa kufanya mambo mengi vizuri zaidi hasa kipindi cha kwanza.

"Tunaweza kucheza vyema na kuhakikisha tunajiandaa dhidi ya Bournemouth, kwa sababu huo utakuwa mchezo mgumu."

Alipoulizwa ni vipi Arsenal wangeweza kupata nguvu ya kiakili inayohitajika kuishinda City hadi kutwaa ubingwa, Arteta alisema: "Ni jambo ambalo tunapaswa kufanya mazoezi na kujadili na kujenga.

"Sio rahisi, lakini wakati mwingi hufanyika kupitia uzoefu na wakati mwingi ni uzoefu ambao hutaki kupitia, lakini kalenda na muundo utatoa hiyo.


"Wakati mwingine uko hapa tulipo sasa, wakati mwingine ni pointi tatu tofauti, pointi mbili, itatokea na lazima tuishi na hilo."

Arsenal watamenyana na Bournemouth walio katika hatari ya kushuka daraja katika mchezo utakaofanyika kesho kabla ya kuelekeza nguvu zao kwenye mechi ya hatua ya 16 bora wa Ligi ya Europa dhidi ya Sporting CP.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,083,8
MSHINDI WA SUPA JACKPOT YA MECHI - 13


KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TEN HAG AKUNWA NA MAGUIRE, WEGHORST



**MANCHESTER, England**

HARRY Maguire na Wout Weghorst wanaendelea kumvutia Erik ten Hag, huku kocha huyo wa Manchester United akiwasifu wawili hao kwa uchezaji wao dhidi ya West Ham.

Wawili hao walianza katika ushindi wa Jumatano wa raundi ya tano ya Kombe la FA kwenye Uwanja wa Old Trafford, wakicheza vizuri wakati wakishinda mabao 3-1 siku chache baada ya kubeba Kombe la Carabao dhidi ya Newcastle.

Nahodha wa timu hiyo Maguire, ambaye alicheza dakika chache za mwisho Wembley pekee, amekuwa hana nafasi mbele ya Raphael Varane na Lisandro Martinez chini ya Ten Hag.

Lakini beki huyo wa kati alionyesha hali iliyomfurahisha kTen Hag huku akifurahi kumwona akizoea kucheza upande wa kulia badala ya kushoto.

"Njia yangu ya kucheza, ni bora," alisema. "Napendelea kuwa na wachezaji wenye nguvu nyingi na alikuwa na kiwango kizuri. Alichukua hatua ya ndani na nje ya kumiliki mpira.

"Alikuwa akihitaji mpira na alikuwa na wakati mzuri sana. Nilimwonyesha video ya uchezaji wake na ya wachezaji wengine jinsi ya kuwazidi wapinzani.

Weghorst, ambaye alianza Wembley na kutoa asisti kwa Marcus Rashford siku ya Jumapili, amekuwa akilaumiwa kwa kukosa kwake mabao tangu alipowasili kwa mkopo kutoka Burnley.

Lakini kazi ya mshambuliaji huyo kugonga mpira inaendelea kumfurahisha Ten Hag, baada ya kuchangia mabao yote matatu ya United siku ya Jumatano, likiwao goli la kujifunga la Nayef Aguerd na Alejandro Garnacho na juhudi za Fred.

# Van Dijk: Liverpool inahitaji nguvu

**LIVERPOOL, England**

VIRGIL van Dijk alipongeza "ushindi muhimu" kwa Liverpool walipowafunga Wolves mabao 2-0 kule Anfield kabla ya kuwakaribisha Manchester United hapo Jumapili ambapo amesema "tutahitaji nguvu zaidi ".

Van Dijk alifunga bao la kwanza huku Wekundu hao dakika ya 73 juzi akiunganisha kwa kichwa krosi ya Diogo Jota kabla ya Mohamed Salah kufunga bao la pili dakika nne baadaye.

"Ushindi muhimu, kwa hivyo ni wakati wa kupona na kuzingatia inayofuata," alisema Van Dijk akiiambia BBC Sport.

"Bila shaka ilibidi tuwe na subira. Nadhani tunaona michezo tuliyocheza dhidi yao msimu huu, imekuwa migumu sana na leo haikuwa tofauti kwa hiyo tulilazimika kuwa na subira na kusubiri muda huo."



Liverpool watacheza na United walio katika kiwango kizuri wakiwa nyumbani, na Van Dijk hana shaka mchezo utakuwa mgumu, ndiyo maana watahitaji msaada wa mashabiki.

"Nadhani tunahitaji mazingira makubwa siku ya Jumapili," alisema.

HABARI MICHEZO


326,057/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/03/23 | 20:30 | Southampton FC vs Leicester City | 2.65 | 3.25 | 2.60 |
| 02. 04/03/23 | 20:30 | Tenerife CD vs SD Eibar | 2.36 | 2.80 | 3.40 |
| 03. 04/03/23 | 20:45 | FC Volendam vs FC Emmen | 2.60 | 3.35 | 2.60 |
| 04. 04/03/23 | 22:45 | ACF Fiorentina vs AC Milan | 2.80 | 3.20 | 2.48 |
| 05. 04/03/23 | 22:45 | Standard Liege vs KVC Westerlo | 2.39 | 3.45 | 2.75 |
| 06. 04/03/23 | 23:00 | CD Mirandes vs Real Oviedo | 2.48 | 2.90 | 3.15 |
| 07. 05/03/23 | 14:30 | Spezia Calcio vs Hellas Verona | 2.75 | 3.10 | 2.60 |
| 08. 05/03/23 | 15:30 | Hansa Rostock vs Karlsruher SC | 2.70 | 3.30 | 2.50 |
| 09. 05/03/23 | 16:00 | Real Valladolid vs Espanyol Barcelona | 2.24 | 3.15 | 3.25 |
| 10. 05/03/23 | 17:00 | Nottingham Forest vs Everton FC | 2.65 | 3.00 | 2.75 |
| 11. 05/03/23 | 19:30 | Liverpool FC vs Manchester United | 2.38 | 3.40 | 2.80 |
| 12. 05/03/23 | 19:30 | VfL Wolfsburg vs Eintracht Frankfurt | 2.43 | 3.40 | 2.75 |
| 13. 05/03/23 | 20:30 | Rayo Vallecano vs Athletic Bilbao | 2.90 | 3.00 | 2.55 |
| 14. 05/03/23 | 21:00 | Santa Clara Azores vs Vitoria SC Guimaraes | 2.70 | 3.15 | 2.60 |
| 15. 05/03/23 | 22:00 | SC Cambuur vs Go Ahead Eagles | 2.75 | 3.30 | 2.47 |
| 16. 05/03/23 | 22:45 | AS Roma vs Juventus Turin | 2.37 | 3.05 | 3.10 |
| 17. 05/03/23 | 22:45 | Stade Rennes vs Olympique Marseille | 2.75 | 3.35 | 2.45 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 03/03/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 17:00 | 4915 | Bologna Youth vs Frosinone Youth | 2.39 | 3.30 | 2.40 |
| 18:00 | 1650 | Coca Cola vs Ismaily SC | 1.95 | 3.15 | 3.94 |
| 19:00 | 4838 | Young Africans vs Tanzania Prisons | 1.15 | 5.00 | 9.00 |
| 19:00 | 4910 | Fakel vs FK Khimki | 1.84 | 3.46 | 3.87 |
| 20:00 | 1221 | Goeztepe vs Boluspor | 2.23 | 3.08 | 2.98 |
| 20:00 | 2066 | Alanyaspor vs Basaksehir | 2.72 | 3.30 | 2.41 |
| 20:00 | 2939 | Pendikspor vs Altinordu | 1.57 | 3.70 | 4.93 |
| 20:00 | 4197 | Congo vs Tunisia | 3.01 | 2.95 | 2.33 |
| 20:30 | 2899 | Moroka Swallows FC vs Orlando Pirates | 3.50 | 2.98 | 2.13 |
| 20:30 | 3289 | Paderborn vs St. Pauli | 2.26 | 3.37 | 2.93 |
| 20:30 | 4214 | Al Nasr Riyadh vs AL Baten | 1.11 | 8.54 | 19.21 |
| 21:00 | 1683 | Aarhus vs Horsens | 1.76 | 3.64 | 4.29 |
| 21:00 | 5508 | Universitatea Cluj vs Farul Constanta | 3.13 | 3.03 | 2.27 |
| 21:00 | 5657 | Red Star Belgrade vs Partizan | 1.77 | 3.30 | 4.12 |
| 21:30 | 1415 | Concarneau vs Cholet | 1.61 | 3.78 | 5.04 |
| 21:30 | 3768 | Le Mans vs Bastia Borgo | 1.40 | 4.32 | 7.16 |
| 21:30 | 4583 | Nancy vs FC Versailles 78 | 2.28 | 3.14 | 3.04 |
| 21:30 | 4795 | Avranches vs Paris 13 Atletico | 2.53 | 3.04 | 2.78 |
| 21:30 | 4902 | Le Puy vs Sedan | 2.74 | 3.01 | 2.58 |
| 21:30 | 5333 | Yverdon vs Sport FC-FC Wil | 2.31 | 3.49 | 2.56 |
| 21:30 | 5518 | Orleans vs Saint Brieuc | 2.17 | 3.10 | 3.31 |
| 22:00 | 1229 | Utrecht vs Fortuna Sittard | 1.52 | 4.22 | 5.10 |
| 22:00 | 2395 | Maastricht vs VVV Venlo | 2.59 | 3.55 | 2.35 |
| 22:00 | 2497 | Dordrecht vs Almere City | 3.59 | 3.49 | 1.89 |
| 22:00 | 2556 | Boavista vs FC Arouca | 2.08 | 3.16 | 3.46 |
| 22:00 | 3964 | Vitesse Arnhem vs AZ Alkmaar | 3.18 | 3.48 | 2.05 |
| 22:00 | 5434 | Telstar vs FC Eindhoven | 2.35 | 3.13 | 2.87 |
| 22:00 | 5817 | PEC Zwolle vs Den Bosch | 1.20 | 6.02 | 10.17 |
| 22:15 | 2443 | Neuchatel Xamax vs FC Aarau | 2.45 | 3.50 | 2.41 |
| 22:15 | 3780 | Ferencvaros TC vs Mezokovesdi SE | 1.27 | 5.09 | 8.73 |
| 22:30 | 2114 | Borussia Dortmund vs RB Leipzig | 2.20 | 3.53 | 2.84 |
| 22:30 | 2837 | SKN St Polten vs SV Horn | 2.00 | 3.47 | 3.21 |
| 22:30 | 3214 | Lech Poznan vs Lechia Gdansk | 1.44 | 4.06 | 5.96 |
| 22:45 | 1103 | Dundalk FC vs St Patricks | 2.55 | 3.09 | 2.53 |
| 22:45 | 1508 | Drogheda Utd vs Sligo Rovers | 3.03 | 3.18 | 2.15 |
| 22:45 | 2251 | Wexford Youths vs Athlone Town | 1.71 | 3.85 | 3.75 |
| 22:45 | 2432 | Hamilton vs Arbroath | 2.44 | 3.17 | 2.70 |
| 22:45 | 3421 | Kerry FC vs Treaty United | 3.08 | 3.39 | 2.04 |
| 22:45 | 3514 | Shelbourne vs Bohemians FC | 2.30 | 2.98 | 2.93 |
| 22:45 | 3838 | Napoli vs Lazio | 1.56 | 3.87 | 5.29 |
| 22:45 | 4120 | Cork City vs UCD Dublin | 1.72 | 3.44 | 4.22 |
| 22:45 | 5515 | Southend vs Barnet | 1.80 | 3.58 | 4.00 |
| 22:45 | 5740 | Oostende vs Brugge | 4.45 | 4.05 | 1.63 |
| 22:45 | 5844 | Waterford Utd vs Galway United | 1.98 | 3.49 | 3.13 |
| 23:00 | 2296 | Real Sociedad vs Cadiz CF | 1.49 | 3.99 | 6.79 |
| 23:00 | 3028 | FC Andorra vs Las Palmas UD | 2.76 | 2.91 | 2.61 |
| 23:00 | 3416 | Hull City vs West Bromwich | 3.04 | 3.14 | 2.26 |
| 23:00 | 3558 | Shamrock Rovers vs Derry City | 2.38 | 3.04 | 2.78 |
| 23:00 | 3805 | Nice vs AJ Auxerre | 1.57 | 3.85 | 5.33 |
| 23:00 | 4834 | Finn Harps vs Bray Wanderers | 2.10 | 3.28 | 3.03 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MWAKINYO ULINGONI APRILI, AFURAHIA UTEUZI MWANA FA

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kimya kirefu bondia, Hassan Mwakinyo, anatarajia kupanda ulingoni Aprili 22, mwaka huu kwenye Uwanja wa Jamhuri, jijini mkoani Dodoma kupigana na bondia kutoka Afrika Kusini.

Pambano hilo limeandaliwa na promota maarufu wa kike nchini, Sophia Mwakagenda, na lengo lake ni kukusanya taulo za kike 40,000 kwa ajili ya kuwapatia wanafunzi mbalimbali wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Mwakagenda alisema tayari wameshaanza mazungumzo na mabondia watakaopigana na Mwakinyo na wanatarajia pambano hilo litakuwa na ubora wa kimataifa kutokana na kushirikisha mabondia nyota wanaume na wanawake.

Mara ya mwisho Mwakinyo kupanda ulingoni ilikuwa Septemba 3, mwaka jana na alipambana na Liam Smith mjini Liverpool na alipoteza pambano hilo kwa TKO katika raundi ya nne.

Naye Mwakinyo alisema anatarajia kurejea kwa nguvu zote pamoja na kutoingia ulingoni kwa miezi zaidi ya mitano.

"Ni kweli sijapigana muda mrefu na mengi yamesemwa, sasa narejea kwa nguvu zote na kufuta mawazo yote hasi dhidi yangu. Kwa kifupi sipigani kwa lengo la kuwafurahisha baadhi ya watu, nafanya hivyo kwa ajili ya kukuza kipaji changu," alisema Mwakinyo.

Aliongeza anampongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa juhudi zake za kuendeleza michezo na kuleta hamasa kubwa.

Alisema kumteua Hamisi Mwinjuma kuwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, itaongeza hamasa katika michezo, sanaa na utamaduni kwa sababu kiongozi huyo anafaa na ni mdau mkubwa wa sekta hiyo.



Mkurugenzi wa Kampuni ya Lady in Red Boxing Promotion, Sophia Mwakagenda (kushoto), akizungumza kuhusu pambano atakalopigana bondia, Hassan Mwakinyo (kulia) litakalofanyika Aprili 22, mwaka huu kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma. Mwakinyo atapambana na bondia kutoka Afrika Kusini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Sinema Fei Toto, Yanga yaendelea

INATOKA UK. 24

anapopataka na haki itendeke na mtoto awe huru kufanya yake," aliongeza mzazi huyo.

Mtine aliliambia gazeti hili Yanga inasubiri uamuzi utakaotolewa baada ya kuitikia wito wa marejeo wa shauri hilo.

Mjumbe wa Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji, Hussein Kitta, alisema wamefanikiwa kusikiliza kwa mara ya pili pande zote mbili na wanatarajia kutoa uamuzi muda wowote kuanzia sasa.

Desemba 24, mwaka jana, Fei Toto alitangaza kuvunja mkataba na Yanga kwa kuiandikia barua klabu hiyo ambayo ilifungua mashtaka ikipinga uamuzi wa kiungo huyo.

## Simba yatinga robo fainali FA

INATOKA UK. 24

Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema atafanya mabadiliko katika mchezo huo kwa lengo la kuwapa nafasi ya kucheza wachezaji ambao wanakosa namba mara kwa mara ndani ya kikosi cha timu hiyo.

Nabi alisema siku zote malengo ya Yanga ni kushinda kila taji la michuano wanayoshiriki na hali hiyo wanahitaji kupata ushindi katika mchezo wa leo.

"Tumejipanga kuhakikisha tunashinda mchezo wa kesho (leo) wa Kombe la FA dhidi ya Tanzania Prisons, Yanga ni timu kubwa na tunahitaji kushinda kila taji na tupo tayari," Nabi alisema.

Naye Kocha Mkuu wa Tanzania Prisons, Mohammed Abdallah 'Bares', alisema wanawaheshimu Yanga na wataingia kwa tahadhari kubwa katika mchezo huo.

Bares alisema Yanga ni timu nzuri yenye wachezaji wazuri lakini wamejipanga kuhakikisha wanafanya vyema katika mchezo wa leo ili kupata matokeo chanya.

"Mechi itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu wote tunahitaji matokeo mazuri, Yanga ni mabingwa watetezi wanahitaji matokeo, hata sisi tunahitaji kushinda hii mechi ili kufuzu hatua ya robo fainali ya michuano hii," alisema Bares.

# Michezo

Ijumaa Machi 3 2023

Nipashe



UKURASA 21

## Arteta: Hatuachi kutafuta ubingwa



Kiungo nyota nchini, Feisal Salum 'Feitoto' (katikati), akitoka kusikiliza shauri linalomhusu dhidi ya Yanga katika kikao kilichoitishwa na Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SIMBA YATINGA ROBO FAINALI FA

## ●●●Leo ni zamu ya Yanga kuwakaribisha Maafande wa Prisons katika...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

STRAIKA chipukizi aliyesajiliwa katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi mwaka huu, Mohammed Mussa, akitokea kwenye klabu ya Malindi alifunga bao lake la kwanza tangu ajiunge na Simba iliyotinga hatua ya robo fainali ya Kombe la FA kwa kuitandika African Sports mabao 4-0 katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana.

Mussa alifunga bao la tatu katika mechi hiyo akiingia kipindi cha pili baada ya kuchukua nafasi ya Habib Kyombo na kupachika bao hilo lililoanzia kwa kipa wa Simba, Beno Kakolanya, aliyemwanzishia mpira, Peter Banda na baadaye Moses Phiri.

Simba ilianza kupiga hodi langoni mwa African Sports dakika ya saba ya mchezo kwa Phiri kuambaa na mpira katika winga ya kushoto na kupiga krosi iliyomkuta, Jean Baleke, ambaye alipiga shuti dhaifu lililopanguliwa na kipa wa African Sports, Hamisi Rajab.

Pape Sakho angeweza kuipatia Simba bao dakika ya 13, alipobaki na kipa wa African Sports, lakini shuti lake lilikosa shabaha na kutoka nje.

Wachezaji wa Africans Sports walianza mechi hiyo kwa staili ya 'kupaki basi' na mfumo huo uliwapa Simba nafasi ya kukaa na mpira muda mrefu, wakipasiana pasi za hapa na pale na kufanya mashambulizi ikiwamo la Israel Mwenda kukaribia kufunga bao dakika ya 25 baada ya kupewa pasi na Sakho lakini shuti lake lilitoka nje.

Phiri naye alikosa bao la wazi akiwa hatua chache tu kutoka langoni mwa African Sports, shuti lake kali likipanguliwa na kipa.

Alikuwa ni Baleke aliyeukwamisha mpira ndani ya wavu dakika ya 35, akipata pasi ndefu katikati ya uwanja kutoka kwa Sakho, akawa anaukimbiza mpira huyo huku kipa Rajab naye akitaka kuuwahi, lakini mfungaji huyo aliuwahi, akaudokoa mpira ukampita kichwani na kujaa wavuni.

Dakika ya pili tu baada ya mpumziko, beki wa kati, Kennedy Juma aliandika bao la pili liliwafanya Africans Sports kubadilisha mfumo kutoka nyuma na kuanza kushambulia, wakimtumia, Wallace Kiango, ambaye alionekana kuichachafya kidogo ngome ya Wekundu wa Msimbazi.

Bao la nne la washindi lilifungwa dakika moja kabla ya mechi kumalizika, kazi nzuri iliyofanywa na Banda kwenye wingi ya kulia ya kuwatoka mabeki na kupiga krosi pasi, iliyotendewa haki na Jimmyson Mwanuke.

Wakati huo huo, mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Yanga inatarajia kuwakaribisha Tanzania Prisons katika mchezo wa hatua ya 16 Bora itakayochezwa kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Yanga itaendelea kukosa huduma ya kiungo wake, Bernard Morrison ambaye bado ni majeruhi huku nyota wengine wa kikosi cha kwanza watakuwa benchi na kuingia kwa dakika chache.

INAENDELEA UK. 23

## Sinema Fei Toto, Yanga yaendelea

**Na Saada Akida**

SAKATA la kiungo, Feisal Salum 'Fei Toto', bado linaendelea baada ya Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kufanya kikao na nyota huyo pamoja na viongozi wa Yanga kuchukua zaidi ya dakika 120.

Kamati hiyo ilianza kikao chake jana saa 5:17 asubuhi na kumalizika saa 7:15 mchana, pande zote mbili zikiondoka katika eneo la tukio, kwenye ofisi za TFF zilizoko Ilala, Karume Dar es Salaam.

Kikao hicho kilihusu marejeo ya hukumu ya mwanzo iliyoamua Fei Toto bado ni mchezaji halali wa Yanga na anapaswa kurejea kikosini huku mchezaji huyo akikataa kukubaliana na uamuzi huo.

Fei Toto alifika TFF saa 4:02 asubuhi na gari aina ya Toyota Alphard yenye namba za usajili T569 DVC akiambatana na mawakili, Fatma Karume, Nduruma Majembe, mama mzazi na ndugu zake.

Yanga iliwakilishwa na Ofisa Mtendaji Mkuu, Andre Mtine, Mkurugenzi wa Sheria, Simon Patrick na mawakili wengine wanne ambao walitinga TFF saa 4:05 asubuhi.

Baada ya kusikilizwa shauri hilo, Fatma alisema Feisal amemwomba kuongeza nguvu katika shauri hilo ili kuhakikisha anapata haki yake kwa kuwa ni mchezaji ambaye anamfahamu na ni mtu wake wa karibu.

"Tumeridhishwa na masikilizo haya, hatuna cha kuzungumza zaidi ya kusubiri maamuzi ya kamati kwa kuwa tuna imani itatenda haki kwetu," Fatma alisema.

Naye mama mzazi wa nyota huyo, Bimkubwa Haroub, alisema anaomba TFF watende haki juu ya suala ya kesi ya mwanawe.

"Naomba TFF itende haki Fei Toto aliyejitolea kucheza Yanga, baada ya kuteseka kwa mtoto huyu ndio amefanya maamuzi haya ya kuondoka Yanga.

Fei Toto sio mwendawazimu na familia kwa ujumla tunahitaji aondoke Yanga kumwachia na aende

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >

Na Adam Fungamw